# Ayubu

## Sehemu ya kwanza: Habari za awali

*(Ayubu 1–2)*

### *Ayubu na jamaa yake*

1 Katika nchi ya Usi paliishi mtu ambaye ali-
itwa Ayubu. Mtu huyu alikuwa hana hatia,
naye alikuwa mkamilifu; alimcha Mungu na
kuepukana na uovu.
2 Alikuwa na wana saba na binti watatu,
3 naye alikuwa na kondoo elfu saba, ngamia
elfu tatu, jozi mia tano za maksai, na punda mia
tano, tena alikuwa na idadi kubwa ya watumishi.
Alikuwa mtu maarufu sana miongoni mwa watu
wa Mashariki.
4 Wanawe walikuwa na desturi ya kufanya
karamu katika nyumba zao kwa zamu, nao
wangewaalika dada zao watatu ili kula na kun-
ywa pamoja nao.
5 Kipindi cha karamu kilipomalizika, Ayubu
angetuma waitwe na kuwafanyia utakaso. Ange-
toa dhabihu ya sadaka ya kuteketezwa kwa ajili
ya kila mmoja wao asubuhi na mapema, akifikiri,
“Pengine wanangu wametenda dhambi na kum-
laani Mungu mioyoni mwao.” Hii ilikuwa ndiyo
desturi ya kawaida ya Ayubu.

### *Jaribu la kwanza la Ayubu*

6 Siku moja wana wa Mungu* walienda ku-
jionesha mbele za Mwenyezi Mungu. Shetani†
naye akaja pamoja nao.
7 Mwenyezi Mungu akamwambia Shetani,
“Umetoka wapi?”

Shetani akamjibu Mwenyezi Mungu, “Natoka kuzunguka duniani, nikitembea huku na huko.”

8 Ndipo Mwenyezi Mungu akamwambia
Shetani, “Je, umemwangalia huyo mtumishi wangu Ayubu? Hakuna mtu mwingine duniani aliye kama yeye, asiye na hatia, ni mnyofu, mwenye kumcha Mungu, na kuepukana na uovu.”
9 Shetani akamjibu Mwenyezi Mungu, “Je,
Ayubu anamcha Mungu bure?
10 Je, wewe hukumzingira pande zote, yeye na
watu wa nyumbani mwake, pamoja na kila kitu alicho nacho? Kazi za mikono yake umezibariki, na hivyo makundi yake ya kondoo na mbuzi pamoja na ya wanyama yameenea katika nchi nzima.
11 Lakini nyoosha mkono wako na kupiga kila
kitu alicho nacho, naye kwa hakika atakulaani mbele za uso wako.”
12 Mwenyezi Mungu akamwambia Shetani,
“Vema sana, kwa hiyo, kila kitu alicho nacho kiko mikononi mwako, lakini huyo mtu mwenyewe usimguse hata kwa kidole.”

Ndipo Shetani akatoka mbele za Mwenyezi Mungu.

* **1:6** *wana wa Mungu* hapa ina maana *malaika* au *viumbe vya mbinguni* † **1:6** yaani *mshtaki wa watakatifu*

13 Siku moja watoto wa Ayubu walipokuwa
wakifanya karamu wakila na kunywa divai
katika nyumba ya ndugu yao mkubwa,
14 akaja mjumbe kwa Ayubu na kusema, “Mak-
sai walikuwa wakilima na punda walikuwa wak-
ilisha karibu nao,
15 Waseba wakawashambulia na kuchukua
mifugo. Kisha wakawaua watumishi kwa up-
anga, mimi peke yangu ndiye niliyenusurika
kukuletea habari!”

16 Alipokuwa bado ananena, mjumbe
mwingine akaja na kusema, “Moto wa Mungu
ulishuka kutoka mbinguni na kuteketeza
kondoo na watumishi, mimi peke yangu ndiye
niliyenusurika kukuletea habari!”

17 Alipokuwa bado ananena, mjumbe
mwingine akaja na kusema, “Wakaldayo
waliunda vikosi vitatu vya uvamizi na
kuwaangukia ngamia wako na kuwachukua
wakaondoka nao. Wakawaua watumishi kwa
upanga, mimi peke yangu ndiye niliyenusurika
kukuletea habari.”

18 Alipokuwa bado ananena, mjumbe
mwingine akaja na kusema, “Wana wako wa
kiume na wa kike walipokuwa wakifanya
karamu, wakila na kunywa divai katika nyumba
ya ndugu yao mkubwa,
19 ghafula upepo wenye nguvu ukavuma ku-
toka jangwani, nao ukaipiga nyumba hiyo pembe
zake nne. Ikawaangukia hao watoto nao wamek-
ufa, mimi peke yangu ndiye niliyenusurika
kukuletea habari!”

20 Ndipo Ayubu akasimama, akararua joho lake
na kunyoa nywele zake. Kisha akasujudu na
kuabudu,
21 akasema:
"Nilitoka tumboni mwa mama yangu uchi,
nami nitaondoka uchi‡,
Mwenyezi Mungu alinipa,
naye Mwenyezi Mungu ameviondoa;
jina la Mwenyezi Mungu litukuzwe."
22 Katika mambo haya yote, Ayubu hakutenda
dhambi kwa kumlaumu Mungu kwa kufanya
ubaya.

# 2

*Jaribu la pili la Ayubu*

1 Siku nyingine wana wa Mungu walienda
kujionesha mbele za Mwenyezi Mungu. Shetani
naye akaja pamoja nao kujionesha mbele zake.
2 Mwenyezi Mungu akamwambia Shetani,
"Umetoka wapi?"

Shetani akamjibu Mwenyezi Mungu, "Natoka kuzunguka duniani, nikitembea huku na huko."
3 Mwenyezi Mungu akamwambia Shetani, "Je,
umemwangalia huyo mtumishi wangu Ayubu?
Hakuna mtu mwingine duniani aliye kama yeye,
mtu asiye na hatia, ni mnyofu, mwenye kumcha
Mungu na kuepukana na uovu. Naye bado
anadumisha uadilifu wake, ingawa ulinichochea
dhidi yake, ili nimwangamize pasipo sababu."

‡ **1:21** au *nitarudi huko uchi*

4 Shetani akamjibu Mwenyezi Mungu, “Ngozi
kwa ngozi! Mwanadamu atatoa vyote alivyo
navyo kwa ajili ya uhai wake.
5 Lakini nyoosha mkono wako na kuipiga
nyama yake na mifupa yake, naye kwa hakika
atakulaani mbele za uso wako.”
6 Mwenyezi Mungu akamwambia Shetani,
“Vema sana; kwa hiyo, yeye yumo mikononi
mwako, lakini lazima umwachie uhai wake.”
7 Basi Shetani akatoka mbele za Mwenyezi
Mungu, naye akampiga Ayubu kwa majipu
mabaya tangu nyayo za miguu yake hadi utosi wa
kichwa.
8 Ndipo Ayubu akachukua kigae na kujikuna
nacho, huku akiketi kwenye majivu.
9 Mke wake akamwambia, “Je, bado unashika-
mana na uadilifu wako? Mlaani Mungu nawe
ukafe!”
10 Akamjibu, “Unazungumza kama mwanamke
mpumbavu*. Je, tupokee mema kutoka kwa
Mungu, bali tusipokee mabaya?”

Katika mambo haya yote, Ayubu hakutenda dhambi katika kusema kwake.

## *Rafiki watatu wa Ayubu*

11 Basi rafiki watatu wa Ayubu, ndio Elifazi
Mtemani, na Bildadi Mshuhi na Sofari Mnaa-
mathi, waliposikia kuhusu taabu yote iliyompata
Ayubu, wakajipanga kutoka nyumbani mwao,
wakakutana ili kwenda kumtuliza katika taabu
hiyo na kumfariji.

* **2:10** maana yake *kupungukiwa maadili*

12 Walipomwona kwa mbali, ilikuwa vigumu kumtambua. Wakaanza kulia kwa sauti kubwa, wakayararua majoho yao na kujirushia mavumbi juu ya vichwa vyao.
13 Kisha wakaketi chini kwenye udongo pamoja na Ayubu kwa siku saba usiku na mchana. Hakuna yeyote aliyesema naye neno, kwa sababu waliona jinsi mateso yake yalivyokuwa makubwa.

# Sehemu ya pili: Mazungumzo ya Ayubu na rafiki zake watatu

## 3

*(Ayubu 3–31)*

### Hotuba ya kwanza ya Ayubu

*Ayubu anailaani siku aliyozaliwa*

1 Baada ya jambo hili, Ayubu akafumbua kinywa chake na kuilaani siku ya kuzaliwa kwake.
2 Kisha akasema:
3 “Siku ya kuzaliwa kwangu na ipotelee mbali,
na usiku ule iliposemekana,
‘Mtoto wa kiume amezaliwa!’
4 Siku ile na iwe giza;
Mungu juu na asiiangalie;
nayo nuru isiiangazie.
5 Giza na kivuli kikuu viikalie tena;
wingu na likae juu yake;
weusi na uifunike nuru yake.
6 Usiku ule na ushikwe na giza nene;
usihesabiwe katika siku za mwaka,
wala usihesabiwe katika siku za mwezi wowote.

7 Usiku ule na uwe tasa;
sauti ya furaha na isisikike ndani yake.
8 Wale wanaozilaani siku na wailaani hiyo siku,
wale walio tayari kumwamsha Lewiathani*.
9 Nyota zake za alfajiri na ziwe giza;
nao ungojee mwanga bila mafanikio,
wala usiione miali
ya mapambazuko,
10 kwa sababu huo usiku haukunifungia
mlango wa tumbo la mama yangu,
ili kuyaficha macho yangu
kutokana na taabu.

11 “Kwa nini sikuangamia wakati wa kuzaliwa?
Kwa nini sikufa nilipokuwa ninatoka tumboni?
12 Kwa nini pakawa na magoti ya kunipokea
na matiti ili nipate kunyonyeshwa?
13 Kwa maana sasa ningekuwa nimepumzika kwa amani.
Ningekuwa nimelala na kupumzika
14 pamoja na wafalme na washauri wa dunia,
waliojijengea mahali ambapo sasa ni magofu,
15 pamoja na watawala waliokuwa na dhahabu,
waliozijaza nyumba zao kwa fedha.
16 Au kwa nini sikufichwa ardhini kama mtoto aliyezaliwa mfu,
kama mtoto mchanga ambaye kamwe hakuuona mwanga?

* **3:8** Lewiathani ni mnyama mkubwa wa baharini mwenye magamba anayefanana na joka kubwa, mwenye umbo la kutisha, asiyeweza kuvuliwa.

17 Huko waovu huacha kusumbua
na huko waliochoka hupumzika.
18 Wafungwa nao hufurahia utulivu wao,
hawasikii tena sauti ya kukemea ya kiongozi wa watumwa.
19 Wadogo kwa wakubwa wamo humo,
na mtumwa ameachiwa huru kutoka kwa bwana wake.

20 “Mbona nuru inawaangazia wale walio taabuni,
na hao wenye uchungu kupewa uhai,
21 wale wanaotamani kifo ambacho hakiji,
wale wanaotafuta kufa zaidi ya kutafuta hazina iliyofichwa,
22 ambao hujawa na furaha,
na hushangilia wanapofika kaburini?
23 Kwa nini uhai hupewa mtu
ambaye njia yake imefichika,
ambaye Mungu amemzingira?
24 Kwa maana kulia kwangu kwa uchungu kwanijia badala ya chakula;
kusononeka kwangu kunamwagika kama maji.
25 Lile nililokuwa nikiogopa limenijia;
lile nililokuwa nikihofia limenipata.
26 Sina amani, wala utulivu;
sina pumziko, bali taabu tu.”

# 4

## *Elifazi anasema: Ayubu ametenda dhambi*

1 Ndipo Elifazi Mtemani akajibu:
2 “Kama mtu akithubutu kuzungumza nawe,

kutakukasirisha?
Lakini ni nani awezaye
kujizuia asiseme?
3 Fikiri jinsi umewafundisha watu wengi,
jinsi umeitia nguvu
mikono iliyokuwa dhaifu.
4 Maneno yako yamewategemeza wale waliojikwaa;
umeyatia nguvu magoti yaliyokuwa dhaifu.
5 Lakini sasa hii taabu imekujia wewe,
nawe unashuka moyo;
imekupiga wewe,
nawe unafadhaika.
6 Je, kumcha Mungu kwako hakupaswi kuwa
ndiyo matumaini yako
na njia zako kutokuwa na lawama
ndilo taraja lako?

7 “Fikiri sasa: Ni mtu yupi asiye na hatia
ambaye aliwahi kuangamia?
Ni wapi wanyofu
waliwahi kuangamizwa?
8 Kwa jinsi mimi nimechunguza,
wale walimao ubaya
na wale hupanda uovu,
huvuna hayo hayo.
9 Kwa pumzi ya Mungu huangamizwa;
kwa mshindo wa hasira zake huangamia.
10 Simba anaweza kunguruma na kukoroma,
lakini bado meno ya simba mkubwa huvunjika.
11 Simba anaweza kuangamia kwa kukosa mawindo,

nao wana wa simba jike hutawanyika.

12 “Neno lililetwa kwangu kwa siri,
masikio yangu yakasikia mnong’ono wake.
13 Katikati ya ndoto za kutia wasiwasi wakati wa usiku,
hapo usingizi mzito uwapatapo wanadamu,
14 hofu na kutetemeka kulinishika
na kufanya mifupa yangu yote itetemeke.
15 Kuna roho aliyepita mbele ya uso wangu,
nazo nywele za mwili wangu zikasimama.
16 Yule roho akasimama,
lakini sikuweza kutambua kilikuwa kitu gani.
Umbo fulani lilisimama mbele ya macho yangu,
kukawa na ukimya kisha nikasikia sauti:
17 ‘Je, binadamu aweza kuwa mwadilifu kuliko Mungu?
Je, mtu aweza kuwa safi kuliko Muumba wake?
18 Ikiwa Mungu hawaamini watumishi wake,
ikiwa yeye huwalaumu malaika wake kwa kukosea,
19 ni mara ngapi zaidi wale wanaoishi katika nyumba
za udongo wa mfinyanzi,
ambazo misingi yake ipo mavumbini,
ambao wamepondwa kama nondo!
20 Kati ya mawio na machweo
huvunjwa vipande vipande;
bila yeyote kutambua,
huangamia milele.
21 Je, kamba za hema lao hazikung’olewa,

hivyo hufa bila hekima?’

# 5

*Elifazi anaendelea*

1 “Itana, ukitaka, lakini ni nani atakayekujibu?
Ni yupi kati ya hao watakatifu utakayemgeukia?
2 Kuweka uchungu moyoni humuua mpumbavu,
nao wivu humchinja mjinga.
3 Mimi mwenyewe nimemwona mpumbavu akistawi,
lakini ghafula nyumba yake ikawa imelaaniwa.
4 Watoto wake wako mbali na usalama,
hushindwa mahakamani bila mtetezi.
5 Wenye njaa huyala mavuno yake,
wakiyatoa hata katikati ya miiba,
nao wenye kiu huitamani sana mali yake.
6 Kwa maana taabu haioti kutoka kwa udongo,
wala ubaya hauchipui kutoka ardhini.
7 Lakini mwanadamu huzaliwa ili kutaabika,
kwa hakika kama cheche za moto zinavyoruka kuelekea juu.

8 “Lakini ingekuwa ni mimi, ningemlalamikia Mungu,
ningeweka shauri langu mbele zake.
9 Yeye hutenda maajabu yasiyoweza kutambuliwa,
miujiza isiyoweza kuhesabika.
10 Yeye huipa nchi mvua,
huyapeleka maji kunyesha mashamba.
11 Huwainua juu wanyonge,

nao wale wanaoomboleza
huinuliwa wakawa salama.
12 Huipinga mipango ya wenye hila,
ili mikono yao isifikie ufanisi.
13 Yeye huwanasa wenye hekima katika hila yao,
nayo mipango ya wadanganyifu huifagilia mbali.
14 Giza huwapata wakati wa mchana;
wakati wa adhuhuri hupapasa kama vile usiku.
15 Humwokoa mhitaji kutokana na upanga ulioko kinywani mwao;
huwaokoa kutokana na makucha ya wenye nguvu.
16 Kwa hiyo maskini analo tarajio,
nao udhalimu hufumba kinywa chake.

17 “Heri mtu yule ambaye Mungu humkanya;
kwa hiyo usidharau adhabu yake Mwenyezi*.
18 Kwa kuwa hutia jeraha, lakini pia huyafunga;
huumiza, lakini mikono yake pia huponya.
19 Kutoka majanga sita atakuokoa;
naam, hata katika saba hakuna dhara litakalokupata wewe.
20 Wakati wa njaa atakukomboa wewe na kifo,
naye katika vita atakukomboa na pigo la upanga.
21 Utalindwa kutokana na kichapo cha ulimi,
wala hutakuwa na sababu ya kuogopa maangamizi yatakapokujia.

* **5:17** Mwenyezi hapa ni jina la Kiebrania *Shaddai* (na kila mahali katika kitabu hiki cha Ayubu).

22 Utayacheka maangamizi na njaa,
wala hutakuwa na sababu ya kuwaogopa
wanyama wakali wa mwituni.
23 Kwa kuwa utakuwa na agano na mawe ya mashamba,
nao wanyama pori watakuwa na amani nawe.
24 Utajua kwamba hema lako li salama;
utahesabu mali yako wala hutakuta chochote kilichopungua.
25 Utajua kuwa watoto wako watakuwa wengi,
nao wazao wako wengi kama majani ya nchi.
26 Utaingia kaburini ukiwa na umri wa uzee mtimilifu,
kama masuke ya ngano yanapokusanywa kwa wakati wake.

27 “Tumelichunguza hili, nalo ni kweli.
Hivyo lisikie na ulitendee kazi.”

# 6

## Hotuba ya pili ya Ayubu

### *Ayubu anajibu: Malalamiko yangu ni ya haki*

1 Kisha Ayubu akajibu:
2 “Laiti uchungu wangu ungeweza kupimwa,
nayo taabu yangu yote ingewekwa kwenye mizani!
3 Kwa kuwa hakika ingekuwa nzito kuliko mchanga wa bahari zote,
kwa hiyo si ajabu maneno yangu yamekuwa ya haraka.
4 Mishale ya Mwenyezi iko ndani yangu,
roho yangu inakunywa sumu yake;

vitisho vya Mungu vimejipanga dhidi yangu.
5 Je, punda-mwitu hulia akiwa na majani,
au fahali hulia akiwa na chakula?
6 Je, chakula kisicho na ladha huliwa bila chumvi,
au upo utamu katika ute mweupe wa yai?
7 Ninakataa kuvigusa;
vyakula vya aina hii hunichukiza.

8 “Laiti ningepata haja yangu,
kwamba Mungu angenijalia hilo nililotarajia,
9 kwamba Mungu angekuwa radhi kuniponda,
kuuachia mkono wake na kunikatilia mbali!
10 Ndipo bado ningekuwa na hii faraja,
furaha yangu katika maumivu makali:
kwamba sikuwa nimeyakana maneno yake yeye Aliye Mtakatifu.

11 “Nina nguvu gani, hata niendelee kutumaini?
Matazamio yangu ni nini,
hata niendelee kuwa mvumilivu?
12 Je, mimi nina nguvu za jiwe?
Je, mwili wangu ni shaba?
13 Je, ninao uwezo wowote wa kujisaidia mimi mwenyewe,
wakati mafanikio yamefukuziwa mbali nami?

14 “Mtu anayekata tamaa angetazamia moyo wa kujitoa wa rafiki zake,
hata akiacha uchaji wa Mwenyezi.
15 Lakini ndugu zangu sio wa kutegemewa,
ni kama vijito vya msimu,

ni kama vijito ambavyo hufurika
16 wakati vimefunikwa barafu iyeyukayo,
ambavyo hujazwa na theluji inayoyeyuka,
17 lakini hukauka majira ya ukame,
na wakati wa hari hutoweka katika mikondo yake.
18 Misafara hugeuka kutoka njia zake;
hukwea kwenda kwenye nchi ya ukiwa na kuangamia.
19 Misafara ya Tema inatafuta maji,
wafanyabiashara wa Sheba wanaosafiri
hutazama kwa matarajio.
20 Wamedhikika, kwa sababu walikuwa na matumaini;
wanafika huko, lakini wanahuzunika
kwa kukosa walichotarajia.
21 Sasa nanyi mmethibitika
kwamba hamna msaada wowote;
mnaona jambo la kutisha,
nanyi mnaogopa.
22 Je, nimewahi kusema, ‘Toeni kitu kwa ajili yangu,
au mnilipie fidia kutoka mali yenu,
23 au niokoeni mikononi mwa adui,
au nikomboeni kutoka makucha ya wasio na huruma’?

24 “Nifundisheni, nami nitakaa kimya;
nioneshe nilikokosea.
25 Tazama yalivyo ya kuumiza maneno ya kweli!
Lakini mabishano yenu yanathibitisha nini?
26 Je, mna maana ya kuyasahihisha ninayosema,
na kuyafanya maneno ya mtu anayekata tamaa kama upepo?

27 Mngeweza hata kupiga kura kwa ajili ya yatima,
na kubadilishana rafiki yenu na mali.

28 “Lakini sasa kuweni na huruma mkaniangalie mimi.
Je, ningeweza kusema uongo mbele zenu?
29 Tulizeni hasira, msiwe wadhalimu;
angalieni tena, kwa maana nimehatarisha uadilifu wangu*.
30 Je, pana uovu wowote mdomoni mwangu?
Je, kinywa changu hakiwezi kupambanua hila?

# 7

*Ayubu anaendelea*

1 “Je, mwanadamu hana kazi ngumu duniani?
Siku zake si kama zile za mtu aliyeajiriwa?
2 Kama mtumwa anavyovionea shauku vivuli vya jioni,
au mtu aliyeajiriwa anavyoungojea mshahara wake,
3 ndivyo nilivyogawiwa miezi ya ubatili,
nami nimeandikiwa huzuni usiku hata usiku.
4 Nilalapo ninawaza, ‘Itachukua muda gani kabla sijaamka?’
Usiku huwa mrefu, nami najigeuzageuza hadi mapambazuko.
5 Mwili wangu umevikwa mabuu na uchafu,
ngozi yangu imetumbuka na kutunga usaha.

* **6:29** au *haki yangu bado inasimama*

### *Ayubu amlilia Mwenyezi Mungu*

6 “Siku zangu zinapita upesi kuliko mtande wa kufuma,
nazo zinafikia mwisho wake bila matumaini.
7 Kumbuka, Ee Mungu, maisha yangu ni kama pumzi;
macho yangu kamwe hayataona tena raha.
8 Lile jicho linaloniona sasa halitaniona tena;
utanitafuta, wala sitakuwepo.
9 Kama vile wingu liondokavyo na kutoweka,
vivyo hivyo yeye ashukaye kaburini* harudi tena.
10 Kamwe harudi tena nyumbani mwake;
wala mahali pake hapatamjua tena.

11 “Kwa hiyo sitanyamaza;
nitanena kutokana na maumivu makuu ya roho yangu,
nitalalama kwa uchungu wa nafsi yangu.
12 Je, mimi ni bahari, au yule mnyama mkubwa wa baharini,
hata uniweke chini ya ulinzi?
13 Ninapofikiri kwamba kitanda changu kitanifariji,
nacho kiti changu cha fahari kitapunguza malalamiko yangu,
14 ndipo wanitisha kwa ndoto
na kunitia hofu kwa maono,
15 hivyo ninachagua kujinyonga na kufa,
kuliko huu mwili wangu.

---

* **7:9** Kaburini maana yake ni *Kuzimu*; kwa Kiebrania ni *Sheol.*

16 Ninayachukia maisha yangu; nisingetamani kuendelea kuishi.
Niache; siku zangu ni ubatili.

17 “Mwanadamu ni kitu gani hata umjali kiasi hiki,
kwamba unamtia sana maanani,
18 kwamba unamwangalia kila asubuhi
na kumjaribu kila wakati?
19 Je, hutaacha kamwe kunitazama,
au kuniacha japo kwa kitambo kidogo tu?
20 Ikiwa nimetenda dhambi, nimekufanyia nini,
Ewe mlinzi wa wanadamu?
Kwa nini umeniweka niwe shabaha yako?
Je, nimekuwa mzigo kwakwo?
21 Kwa nini husamehi makosa yangu
na kuachilia dhambi zangu?
Kwa kuwa hivi karibuni nitalala mavumbini;
nawe utanitafuta, wala sitakuwepo.”

# 8

### *Bildadi anasema: Yampasa Ayubu atubu*

1 Kisha Bildadi Mshuhi akajibu:
2 “Hata lini wewe utasema mambo kama haya?
Maneno yako ni kama upepo mkuu.
3 Je, Mungu hupotosha hukumu?
Je, Mwenyezi hupotosha kile kilicho haki?
4 Watoto wako walipomtenda dhambi,
aliwapa adhabu ya dhambi yao.
5 Lakini ukimtafuta Mungu,
nawe ukamsihi Mwenyezi,
6 ikiwa wewe ni safi na mnyofu,

hata sasa atainuka mwenyewe kwa niaba yako,
na kukurudisha katika mahali pako pa haki.
7 Ijapokuwa mwanzo wako ulikuwa mdogo,
lakini mwisho wako utakuwa wa mafanikio.

8 “Ukaulize vizazi vilivyotangulia
na uone baba zao walijifunza nini,
9 kwa kuwa sisi tumezaliwa jana tu na hatujui lolote,
nazo siku zetu duniani ni kama kivuli tu.
10 Je, hawatakufundisha na kukueleza?
Je, hawataleta maneno ya ufahamu wao?
11 Je, mafunjo yaweza kumea mahali pasipo na matope?
Matete yaweza kustawi bila maji?
12 Wakati bado yanaendelea kukua kabla ya kukatwa,
hunyauka haraka kuliko majani mengine.
13 Huu ndio mwisho wa watu wote wanaomsahau Mungu;
vivyo hivyo matumaini ya wasiomjali Mungu huangamia.
14 Lile analolitumainia huvunjika upesi;
lile analolitegemea ni utando wa buibui.
15 Huutegemea utando wake, lakini hausimami;
huung’ang’ania, lakini haudumu.
16 Yeye ni kama mti ulionyeshewa vizuri wakati wa jua,
ukieneza machipukizi yake bustanini;
17 huifunganisha mizizi yake kwenye lundo la mawe,
na kutafuta nafasi kati ya mawe.

18 Unapong'olewa kutoka mahali pake,
ndipo mahali pale huukana na kusema,
'Mimi kamwe sikukuona.'
19 Hakika uhai wake hunyauka,
na kutoka udongoni mimea mingine huota.

20 "Hakika Mungu hamkatai mtu asiye na hatia,
wala kuitia nguvu mikono ya mtenda maovu.
21 Bado atakijaza kinywa chako na kicheko,
na midomo yako na kelele za shangwe.
22 Adui zako watavikwa aibu,
nayo mahema ya waovu hayatakuwepo tena."

# 9

## Hotuba ya tatu ya Ayubu

*Ayubu anajibu: Hakuna Mpatanishi*

1 Kisha Ayubu akajibu:
2 "Naam, najua hili ni kweli.
Lakini mwanadamu awezaje kuwa mwadilifu mbele za Mungu?
3 Ingawa mtu angetaka kushindana naye,
hangeweza kumjibu Mungu hata mara moja miongoni mwa elfu moja.
4 Hekima yake ni kubwa sana na ana uwezo mwingi mno.
Ni nani aliyempinga naye akawa salama?
5 Aiondoa milima bila yenyewe kujua
na kuipindua kwa hasira yake.
6 Aitikisa dunia kutoka mahali pake
na kuzifanya nguzo zake zitetemeke.
7 Husema na jua, nalo likaacha kuangaza;
naye huizima mianga ya nyota.

8 Yeye peke yake huzitandaza mbingu
na kuyakanyaga mawimbi ya bahari.
9 Yeye ndiye Muumba wa nyota za Dubu*, na Orioni†,
Kilimia‡, na makundi ya nyota za kusini.
10 Hutenda maajabu yasiyopimika,
miujiza isiyoweza kuhesabiwa.
11 Anapopita karibu nami, siwezi kumwona;
apitapo mbele yangu, simtambui.
12 Anapochukua kwa ghafula, ni nani awezaye kumzuia?
Ni nani awezaye kumwambia, 'Unafanya nini?'
13 Mungu hataizuia hasira yake;
hata jeshi kubwa la Rahabu§ lenye nguvu
linajikunyata miguuni pake.

14 "Ni vipi basi mimi nitaweza kubishana naye?
Nawezaje kupata maneno ya kuhojiana naye?
15 Ingawa sikuwa na hatia, sikuweza kumjibu;
ningeweza tu kumsihi Mhukumu wangu anihurumie.
16 Hata kama ningemwita kwenye shauri, naye akakubali,
siamini kama angenisikiliza.
17 Yeye angeniangamiza kwa dhoruba
na kuongeza majeraha yangu pasipo na sababu.
18 Asingeniacha nipumue

---

* **9:9** Dubu ni kundi la nyota za kaskazini; pia zinaitwa *Dubu Mkuu.* † **9:9** Orioni ni kundi la nyota kubwa. ‡ **9:9** Kilimia ni kundi la nyota saba. § **9:13** yaani *Misri* kwa fumbo

bali angenifunika kabisa na huzuni kuu.
19 Kama ni suala la nguvu, yeye ni mwenye nguvu!
Kama ni suala la haki, ni nani awezaye kumwita mahakamani?
20 Hata kama sikuwa na hatia, kinywa changu kingenihukumu;
kama sikuwa na kosa, kingenitangaza kuwa mwenye hatia.

21 “Ingawa mimi sina kosa,
haileti tofauti katika nafsi yangu;
nauchukia uhai wangu.
22 Hayo yote ni sawa; ndiyo sababu nasema,
‘Yeye huwaangamiza wasio na makosa pamoja na waovu.’
23 Wakati wa pigo liletapo kifo cha ghafula,
yeye hudhihaki kule kukata tamaa kwa yule asiye na kosa.
24 Nchi inapoangukia mikononi mwa waovu,
yeye huwafunga macho mahakimu wake.
Kama si yeye, basi ni nani?

25 “Siku zangu zapita mbio kuliko mkimbiaji;
zinapita upesi bila kuona furaha hata kidogo.
26 Zinapita upesi kama mashua ya mafunjo,
mfano wa tai ayashukiaye mawindo kwa ghafula.
27 Nikisema, ‘Nitayasahau malalamiko yangu,
nitabadili sura ya uso wangu na kutabasamu,’
28 bado ninahofia mateso yangu yote,

kwa kuwa ninajua hutanihesabu kuwa sina hatia.
29 Kwa kuwa nimeonekana mwenye hatia,
kwa nini basi nitaabishwe bure?
30 Hata kama ningejiosha kwa sabuni
na kutakasa mikono yangu kwa magadi,
31 wewe ungenitupa kwenye shimo la utelezi
kiasi kwamba hata nguo zangu zingenichukia sana.

32 "Yeye si mwanadamu kama mimi ili niweze kumjibu,
ili tuweze kushindana naye mahakamani.
33 Laiti pangekuwa na mtu wa kutupatanisha,
aweke mkono wake juu yetu sote wawili,
34 mtu wa kuondoa fimbo ya Mungu juu yangu,
ili utisho wake usiendelee kunitia hofu.
35 Ndipo ningenena naye, bila kumwogopa,
lakini kama ilivyo kwangu sasa, sitaweza.

# 10

### *Ayubu anaendelea*

1 "Nayachukia sana haya maisha yangu;
kwa hiyo nitatoa malalamiko yangu kwa wazi bila kujizuia,
nami nitanena kutokana na uchungu wa moyo wangu.
2 Nitamwambia Mungu: Usinihukumu,
bali niambie una mashtaka gani dhidi yangu.
3 Je, inakupendeza wewe kunidhulumu,
kuikataa kazi ya mikono yako,
huku ukiunga mkono mipango ya waovu?
4 Je, wewe una macho ya kimwili?

Je, wewe huona kama mwanadamu aonavyo?
5 Je, siku zako ni kama zile za mwanadamu,
au miaka yako ni kama ile ya mtu,
6 ili utafute makosa yangu
na kuichunguza dhambi yangu;
7 ingawa unajua kuwa mimi sina hatia,
na hakuna awezaye kunitoa mkononi mwako?

8 “Mikono yako ndiyo iliyoniumba na kunifanya.
Je, sasa utageuka na kuniangamiza?
9 Kumbuka kuwa ulinifinyanga kama udongo wa mfinyanzi.
Je, sasa utanifanya kuwa mavumbi tena?
10 Je, wewe hukunimimina mimi kama maziwa,
na kunigandisha kama jibini,
11 ukanivika ngozi na nyama,
na kuniunga pamoja kwa mifupa na mishipa?
12 Umenipa uhai na kunitendea wema,
katika uangalizi wako umeilinda roho yangu.

13 “Lakini hili ndilo ulilolificha moyoni mwako,
nami ninajua kuwa hili lilikuwa katika nia yako:
14 Kama nilifanya dhambi, ungekuwa umeniona,
wala usingeacha kosa langu lipite bila kuadhibiwa.
15 Kama nina hatia, ole wangu!
Hata kama ningekuwa sina hatia,
siwezi kukiinua kichwa changu,
kwa kuwa nimejawa na aibu,

na kuzama katika mateso yangu.
16 Nikiinua kichwa changu juu, unaniwinda kama simba,
na kuonesha tena uwezo wa kutisha dhidi yangu.
17 Wewe waleta mashahidi wapya dhidi yangu
na kuzidisha hasira yako juu yangu;
nazo nguvu zako zinanijia wimbi moja baada ya jingine.

18 “Kwa nini basi ulinitoa tumboni?
Ninatamani ningekufa kabla jicho lolote halijaniona.
19 Laiti nisingezaliwa,
au kama ningepelekwa kaburini
moja kwa moja kutoka tumboni!
20 Je, siku zangu chache si zimekaribia kwisha?
Niachie ili niweze kupata muda mfupi wa kufurahi
21 kabla sijaenda mahali ambapo hakuna kurudi tena,
katika nchi ya giza na uvuli wa mauti,
22 nchi ya giza nene sana,
yenye uvuli wa giza na machafuko,
ambapo hata nuru ni giza.”

# 11

*Sofari anasema: Hatia ya Ayubu inastahili adhabu*

1 Ndipo Sofari Mnaamathi akajibu:
2 “Je, maneno haya yote yapite bila kujibiwa?
Je, huyu mnenaji athibitishwe kuwa na haki?

3 Je, maneno yako ya upuzi yawafanye watu wanyamaze kimya?
Je, mtu asikukemee unapofanya dhihaka?
4 Unamwambia Mungu, ‘Imani yangu ni kamili
nami ni safi mbele zako.’
5 Aha! Laiti kwamba Mungu angesema,
kwamba angefungua midomo yake dhidi yako,
6 naye akufunulie siri za hekima,
kwa kuwa hekima ya kweli ina pande mbili.
Ujue hili: Mungu amesahau hata baadhi ya dhambi zako.

7 “Je, unaweza kujua siri za Mungu?
Je, unaweza kuyachunguza mambo yote kumhusu Mwenyezi?
8 Ni juu mno kuliko mbingu: unaweza kufanya nini?
Kina chake ni kirefu kuliko Kuzimu*:
wewe unaweza kujua nini?
9 Kipimo chake ni kirefu kuliko dunia,
nacho ni kipana kuliko bahari.

10 “Akija na kukufunga gerezani,
na kuitisha mahakama, ni nani awezaye kumpinga?
11 Hakika anawatambua watu wadanganyifu;
naye aonapo uovu, je, haangalii?
12 Mpumbavu aweza kuwa mwenye hekima,
endapo mtoto wa punda-mwitu atazaliwa mwanadamu.

* **11:8** Kuzimu kwa Kiebrania ni *Sheol*, yaani *Shimo lisilo na mwisho.*

13 “Hata sasa ukiutoa moyo wako kwake
na kumwinulia mikono yako,
14 ukiiondolea mbali ile dhambi iliyo mkononi mwako,
wala usiuruhusu uovu ukae kwenye hema lako,
15 ndipo utainua uso wako bila aibu;
utasimama imara bila hofu.
16 Hakika utaisahau taabu yako,
utaikumbuka tu kama maji yaliyokwisha kupita.
17 Maisha yako yatang’aa kuliko adhuhuri,
nalo giza litakuwa kama alfajiri.
18 Utakuwa salama, kwa kuwa lipo tumaini;
utatazama pande zote na kupumzika kwa salama.
19 Utalala, wala hakuna atakayekuogofya,
naam, wengi watajipendekeza kwako.
20 Bali macho ya waovu hayataona,
wokovu utawaepuka;
tarajio lao litakuwa ni hangaiko
la mtu anayekata roho.”

# 12
## Hotuba ya nne ya Ayubu

### *Ayubu anajibu: Mimi ni mtu wa kuchekwa*

1 Ndipo Ayubu akajibu:
2 “Bila shaka ninyi ndio watu,
nayo hekima itakoma mtakapokufa!
3 Lakini mimi ninao ufahamu kama ninyi;
mimi si duni kwenu.
Ni nani asiyejua mambo haya yote?

4 “Nimekuwa mtu wa kuchekwa na rafiki zangu,
ingawa nilimwita Mungu naye akanijibu:
mimi ni mtu wa kuchekwa tu,
ingawa ni mwadilifu na nisiye na hatia!
5 Wanadamu wakiwa katika utulivu huwa na dharau kwa wale wenye msiba
kana kwamba ndiyo haki ya wale ambao miguu yao inateleza.
6 Mahema ya wanyang’anyi hayasumbuliwi,
wale wanaomghadhibisha Mungu wako salama:
wale wamchukuao mungu wao mikononi mwao.

7 “Lakini ulizeni wanyama, nao watawafundisha,
au ndege wa angani, nao watawaambia;
8 au zungumzeni na dunia, nayo itawafundisha,
au acheni samaki wa baharini wawape taarifa.
9 Ni nani miongoni mwa hawa wote asiyejua
kwamba mkono wa Mwenyezi Mungu ndio uliofanya hili?
10 Mkononi mwake kuna uhai wa kila kiumbe,
na pumzi ya wanadamu wote.
11 Je, sikio haliyajaribu maneno
kama vile ulimi uonjavyo chakula?
12 Je, hekima haipatikani kwa wazee?
Je, maisha marefu hayaleti ufahamu?

13 “Hekima na nguvu ni vya Mungu;
shauri na ufahamu ni vyake yeye.
14 Kile anachokibomoa hakiwezi kujengeka tena;
mtu aliyefungiwa naye hawezi kufunguliwa.

15 Akizuia maji, huwa pana ukame;
akiyaachia maji, huharibu nchi.
16 Kwake kuna nguvu na ushindi;
anayedanganywa na anayedanganya, wote wawili ni wake.
17 Yeye huwaondoa washauri wakiwa wametekwa nyara,
naye huwapumbaza wanaotoa maamuzi.
18 Huondoa pingu zilizofungwa na wafalme,
na kuwafunga mishipi ya kiunoni.
19 Huwaondoa makuhani wakiwa wametekwa nyara,
na kuwaangusha waliojiimarisha muda mrefu.
20 Hunyamazisha midomo ya washauri wanaoaminika,
na kuondoa busara ya wazee.
21 Huwadharau wanaoheshimika,
na kuwavua silaha wenye nguvu.
22 Hufunua mambo ya ndani ya gizani,
na kuyaleta nuruni yale yaliyositirika sana.
23 Huyafanya mataifa yatukuke na kuyaangamiza;
hufanya mataifa kuwa makubwa, naye huyatawanya.
24 Huwaondolea viongozi wa nchi akili zao;
huwapeleka watangetange nyikani pasipo na njia.
25 Hupapasa gizani pasipokuwa na mwanga;
huwafanya wapepesuke kama walevi.

# 13

*Ayubu anaendelea*

1 “Macho yangu yameona hili lote,
masikio yangu yamesikia na kulielewa.
2 Hayo mnayoyajua mimi pia ninayajua;
mimi si mtu duni kuliko ninyi.
3 Lakini ninayo shauku ya kuzungumza na Mwenyezi
na kuhojiana shauri langu na Mungu.
4 Ninyi, hata hivyo, hunipakaza uongo;
ninyi ni matabibu wasiofaa kitu, ninyi nyote!
5 Laiti wote mngenyamaza!
Kwa kuwa kwenu hilo lingekuwa hekima.
6 Sikieni sasa hoja yangu;
sikilizeni kusihi kwangu.
7 Je, mtazungumza kwa uovu kwa niaba ya Mungu?
Je, mtazungumza kwa udanganyifu kwa niaba yake?
8 Mtamwonesha upendeleo?
Mtamtetea Mungu kwenye mashtaka yake?
9 Je, ingekuwa vyema
Mungu akiwahoji ninyi?
Je, mngeweza kumdanganya kama ambavyo
mngeweza kuwadanganya wanadamu?
10 Hakika angewakemea
mkiwapendelea watu kwa siri.
11 Je, huo ukuu wake haungewatisha ninyi?
Je, hofu yake isingewaangukia ninyi?
12 Maneno yenu ni mithali za majivu;
utetezi wenu ni ngome za udongo wa mfinyanzi.

13 “Nyamazeni kimya nipate kusema;

kisha na yanipate yatakayonipata.
14 Kwa nini nijiweke mwenyewe kwenye hatari
na kuyaweka maisha yangu mikononi mwangu?
15 Ingawa ataniua, bado nitamtumaini;
hakika nitazitetea njia zangu mbele zake.
16 Naam, hili litanigeukia kuwa wokovu wangu,
kwa maana hakuna mtu asiyemcha Mungu
atakayethubutu kuja mbele yake!
17 Sikilizeni maneno yangu kwa makini;
nayo masikio yenu yaingize kile nisemacho.
18 Sasa kwa kuwa nimekwisha tayarisha kesi yangu,
ninajua nitahesabiwa kuwa haki.
19 Je, kuna yeyote anayeweza kuleta mashtaka dhidi yangu?
Kama ndivyo, nitanyamaza na nife.

20 “Ee Mungu, unijalie tu mimi haya mambo mawili,
nami sitajificha uso wako:
21 Ondoa mkono wako uwe mbali nami,
uache kuniogofya kwa vitisho vyako.
22 Niite kwenye shauri nami nitajibu,
au niache niseme, nawe upate kujibu.
23 Ni makosa na dhambi ngapi nilizotenda?
Nioneshe kosa langu na dhambi yangu.
24 Kwa nini kuuficha uso wako
na kunihesabu mimi kuwa adui yako?
25 Je, utaliadhibu jani lipeperushwalo na upepo?
Je, utayasaka makapi makavu?
26 Kwa kuwa unaandika mambo machungu dhidi yangu

na kunifanya nizirithi dhambi za ujana wangu.
27 Umeifunga miguu yangu kwenye pingu.
Unazichunga kwa makini njia zangu zote
kwa kutia alama kwenye nyayo za miguu yangu.

28 “Hivyo mwanadamu huangamia kama kitu kilichooza,
kama vazi lililoliwa na nondo.

# 14

*Ayubu anaendelea*

1 “Mwanadamu aliyezaliwa na mwanamke
siku zake ni chache nazo zimejaa taabu.
2 Huchanua kama ua kisha hunyauka;
huwa kama kivuli kipitacho upesi, wala hadumu.
3 Je, unamwekea jicho lako mtu kama huyo?
Je, utamleta mbele yako katika hukumu?
4 Ni nani awezaye kutoa kitu safi kutoka kitu najisi?
Hakuna awezaye!
5 Siku za mwanadamu zimewekewa mpaka;
umekwisha kutangaza idadi ya miezi yake
na kuweka mpaka ambao hawezi kuuvuka.
6 Hivyo angalia mbali umwache,
hadi awe amekamilisha muda wake
kama mtu aliyeajiriwa.

7 “Kwa maana lipo tumaini kwa mti;
kama ukikatwa utachipuka tena,
nayo machipukizi yake mapya hayatakoma.

8 Mizizi yake yaweza kuchakaa ardhini
na kisiki chake kufa udongoni,
9 lakini kwa kupata dalili ya maji utachipua
na kutoa machipukizi kama mche.
10 Lakini mwanadamu hufa, na huo ndio mwisho wake;
hutoa pumzi ya mwisho, naye hayuko tena!
11 Kama vile maji yanavyotoweka katika bahari,
au mkondo wa mto ukaushwavyo na kuwa mkavu,
12 ndivyo mwanadamu alalavyo chini asiamke;
hadi mbingu zitakapokuwa hazipo tena,
wanadamu hawataamka au kuamshwa
kutoka usingizi wao.

13 "Laiti kama ungenificha kaburini*,
na kunisitiri hadi hasira yako ipite!
Laiti ungeniwekea wakati,
na kisha ukanikumbuka!
14 Je, kama mtu akifa, aweza kuishi tena?
Siku zote za kazi zangu ngumu
nitangojea kufanywa upya kwangu.
15 Utaniita nami nitakuitika;
utakionea shauku kiumbe ambacho mikono yako ilikiumba.
16 Hakika ndipo utakapozihesabu hatua zangu,
lakini hutazifuatia dhambi zangu.
17 Makosa yangu yatatiwa muhuri kwenye mfuko,
nawe utazifunika dhambi zangu.

* **14:13** Kaburini maana yake ni *Kuzimu*; kwa Kiebrania ni *Sheol*.

18 “Lakini kama mlima umomonyokavyo na kufikichika
na kama vile mwamba uondolewavyo mahali pake,
19 kama maji yamalizavyo mawe,
na mafuriko yachukuavyo udongo,
ndivyo unavyoharibu tegemeo la mwanadamu.
20 Humshinda mara moja kwa daima, naye hutoweka;
waibadilisha sura yake na kumwondoa.
21 Kama wanawe wakipewa heshima, yeye hafahamu;
kama wazao wake wakidharauliwa, yeye haoni.
22 Yeye hasikii kingine isipokuwa maumivu ya mwili wake mwenyewe,
naye huomboleza kwa ajili yake mwenyewe.”

# 15

### *Elifazi anasema: Ayubu anadhoofisha imani*

1 Kisha Elifazi Mtemani akajibu:
2 “Je, mtu mwenye hekima hujibu kwa mawazo matupu,
au kujaza tumbo lake kwa upepo wenye joto wa mashariki?
3 Je, aweza kubishana kwa maneno yasiyofaa,
kwa hotuba zisizo na maana?
4 Lakini unadhoofisha hata uchaji wa Mungu
na kuzuia ibada mbele za Mungu.
5 Dhambi yako inasukuma kinywa chako,
nawe umechagua ulimi wa hila.

6 Kinywa chako mwenyewe kinakuhukumu, wala si changu;
midomo yako mwenyewe inashuhudia dhidi yako.

7 “Je, wewe ni mtu wa kwanza kuzaliwa?
Ulizaliwa kabla ya vilima?
8 Je, wewe husikiliza mashauri ya siri ya Mungu?
Je, wewe unaizuia hekima iwe yako mwenyewe?
9 Wewe unajua kitu gani tusichokijua sisi?
Unafahamu kitu gani tusichokifahamu sisi?
10 Wale wenye mvi na wazee wako upande wetu,
watu ambao ni wazee hata kuliko baba yako.
11 Je, faraja za Mungu hazikutoshi,
au maneno yaliyosemwa kwako kwa upole si kitu?
12 Kwa nini moyo wako unakudanganya,
na kwa nini macho yako yanang’aa,
13 ili upate kutoa hasira yako dhidi ya Mungu,
na kumwaga maneno kama hayo kutoka kinywani mwako?

14 “Mwanadamu ni kitu gani,
hata aweze kuwa safi,
au yeye aliyezaliwa na mwanamke,
hata aweze kuwa mwadilifu?
15 Kama Mungu hawaamini watakatifu wake,
kama hata mbingu zenyewe si safi machoni pake,
16 sembuse mwanadamu ambaye ni mwovu na mpotovu,
ambaye hunywa uovu kama anywavyo maji!

17 “Nisikilize mimi nami nitakueleza,
acha nikuambie yale niliyoyaona,
18 ambayo watu wenye hekima wameyanena,
bila kuficha lolote walilopokea toka kwa baba zao
19 (wakati ambao wao peke yao ndio walipewa nchi,
hakuna mgeni aliyepita miongoni mwao):
20 Mtu mwovu siku zake zote hupata mateso,
miaka yote aliwekewa mkorofi.
21 Sauti za kutisha hujaa masikioni mwake;
katika kufanikiwa kwake, wanyang’anyi humshambulia.
22 Hukata tamaa kuokoka gizani;
amewekwa kwa ajili ya upanga.
23 Hutangatanga, akitafuta chakula;
anajua kwamba siku ya giza iko karibu.
24 Taabu na maumivu makuu vinamtia hofu;
humshinda kama mfalme aliye tayari kwa vita,
25 kwa sababu amemkunjia Mungu ngumi yake
na kujigamba dhidi ya Mwenyezi,
26 kwa kiburi akishambulia dhidi ya Mungu
akiwa na ngao nene, iliyo imara.

27 “Ingawa uso wake umefunikwa na mafuta kwa unene
na kiuno chake kimevimba kwa kunenepa,
28 ataishi katika miji ya magofu,
na katika nyumba ambazo haziishi mwanadamu yeyote,
nyumba zinazokuwa vifusi.
29 Hatatajirika tena, nao utajiri wake hautadumu,

wala mali yake haitakuwa nyingi juu ya nchi.
30 Hatatoka gizani;
mwali wa moto utanyausha machipukizi yake,
nayo pumzi ya kinywa cha Mungu itamwondolea mbali.
31 Asijidanganye mwenyewe kutumainia ubatili,
kwa kuwa hatapata malipo yoyote.
32 Atakuwa amelipwa kikamilifu kabla ya wakati wake,
nayo matawi yake hayatastawi.
33 Atafanana na mzabibu uliopukutishwa matunda yake kabla hayajaiva,
kama mzeituni unaodondosha maua yake.
34 Kwa kuwa jamii ya wasiomcha Mungu watakuwa tasa,
nao moto utateketeza mahema ya wale wanaopenda rushwa.
35 Hutunga mimba ya madhara na kuzaa uovu;
tumbo zao huumba udanganyifu."

# 16
## Hotuba ya tano ya Ayubu

*Ayubu anajibu: Hakika sina hatia*

1 Kisha Ayubu akajibu:
2 "Nimepata kusikia mambo mengi kama haya,
nanyi nyote ni wafariji wenye kutaabisha!
3 Je, maneno yenu mengi yasiyo na maana hayana mwisho?
Mna nini hata mwendelee kushindana kwa maneno?
4 Mimi pia ningeweza kuzungumza kama ninyi,
kama mngekuwa katika hali yangu;

ningeweza kutoa hotuba nzuri dhidi yenu,
na kuwatikisia ninyi kichwa changu.
5 Lakini kinywa changu kingewatia moyo;
faraja kutoka mdomoni mwangu ingewaletea nafuu.

6 “Lakini nikisema, maumivu yangu bado hayatulizwi;
na nikijizuia, bado hayaondoki.
7 Ee Mungu, hakika umenichakaza;
umewaangamiza kabisa watu wa nyumbani mwangu wote.
8 Umenikunjakunja, nalo limekuwa ushahidi;
nako kukonda kwangu kumeongezeka sana na kushuhudia dhidi yangu.
9 Mungu amenishambulia na kunirarua katika hasira yake,
na kunisagia meno yake;
adui yangu hunikazia macho yake makali.
10 Watu wamenifumbulia vinywa vyao kunidhihaki;
hunipiga shavuni mwangu kwa dharau,
na kuungana pamoja dhidi yangu.
11 Mungu amenigeuzia kwa watu wapotovu,
na kunitupa katika makucha ya waovu.
12 Mambo yote yalikuwa mazuri, lakini alinivunjavunja;
amenikamata shingo na kuniponda.
Amenifanya mimi kuwa shabaha yake;
13 wapiga upinde wake wananizunguka.
Bila huruma, huchoma figo zangu,
na kuimwaga nyongo yangu juu ya nchi.
14 Huniponda tena na tena;

hunishambulia kama shujaa wa vita.

15 “Nimejishonea gunia juu ya mwili wangu,
nami nimezika paji la uso wangu kwenye vumbi.
16 Uso wangu umekuwa mwekundu kwa kulia,
macho yangu yamepigwa na giza.
17 Hata hivyo mikono yangu haijafanya jeuri,
na maombi yangu ni safi.

18 “Ee nchi, usiifunike damu yangu,
nacho kilio changu kisinyamazishwe kamwe.
19 Hata sasa shahidi wangu yuko mbinguni;
wakili wangu yuko juu.
20 Mwombezi wangu ni rafiki yangu
macho yangu yanapomwaga machozi kwa Mungu;
21 kwa niaba ya mtu anamsihi Mungu
kama mtu anavyosihi kwa ajili ya rafiki yake.

22 “Ni miaka michache tu itapita
kabla sijaenda safari ambayo sitarudi.

# 17

1 Moyo wangu umevunjika,
siku zangu zimefupishwa,
kaburi linaningojea.
2 Hakika wenye mizaha wamenizunguka;
macho yangu yamebaki kutazama uadui wao.

### *Ayubu anaomba msaada*

3 “Ee Mungu, nipe dhamana unayodai.
Ni nani mwingine atakayeweka dhamana kwa ajili yangu?
4 Umezifunga akili zao zisipate ufahamu,
kwa hiyo hutawaacha wapate ushindi.
5 Kama mtu akiwashutumu rafiki zake ili apate ujira,
macho ya watoto wake yatashindwa kuona.

6 “Mungu amenifanya kitu cha dhihaka kwa kila mtu,
mtu ambaye watu humtemea mate usoni.
7 Macho yangu yamefifia kwa ajili ya majonzi;
umbile langu lote ni kama kivuli.
8 Watu wanyofu wanatishwa na hili;
watu wasio na hatia wanasimama dhidi ya wasiomcha Mungu.
9 Hata hivyo, waadilifu watazishika njia zao,
nao wale wenye mikono safi wataendelea kupata nguvu.

10 “Lakini ninyi njooni, ninyi nyote, jaribuni tena!
Sitampata mtu mwenye hekima miongoni mwenu.
11 Siku zangu zimepita, mipango yangu imevunjika,
vivyo hivyo shauku za moyo wangu.
12 Watu hawa hufanya usiku kuwa mchana,
kwenye giza wao husema, ‘Mwanga u karibu.’
13 Kama nyumba pekee ninayoitarajia ni kaburi*,

* **17:13** Kaburi hapa maana yake ni *Kuzimu*; kwa Kiebrania ni *Sheol.*

nikikitandika kitanda changu gizani,
14 nikiuambia uharibifu, ‘Wewe u baba yangu,’
na kuliambia buu, ‘Wewe u mama yangu’ au ‘Dada yangu,’
15 liko wapi basi tarajio langu?
Ni nani awezaye kuona tarajio lolote kwa ajili yangu?
16 Je, litashuka chini hadi kwenye malango ya mauti†?
Je, tutashuka pamoja mavumbini?”

# 18

*Bildadi anasema: Mwenyezi Mungu huwaadhibu waovu*

1 Bildadi Mshuhi akajibu:
2 “Je, ni lini utafika mwisho wa maneno haya?
Uwe mwenye busara, nasi ndipo tutakapoweza kuongea.
3 Kwa nini sisi tunafikiriwa kama wanyama,
na kuonekana wajinga machoni pako?
4 Wewe unayejirarua mwenyewe vipande vipande
katika hasira yako,
je, dunia iachwe kwa ajili yako wewe?
Au ni lazima miamba iondolewe mahali pake?

5 “Taa ya mwovu imezimwa,
nao mwali wa moto wake umezimika.
6 Mwanga kwenye hema lake umekuwa giza;
taa iliyo karibu naye imezimika.

† **17:16** malango ya mauti hapa ina maana ya *Kuzimu*

7 Nguvu za hatua zake zimedhoofishwa;
hila zake mwenyewe zinamwangusha.
8 Miguu yake imemsukumia kwenye wavu,
naye anatangatanga kwenye matundu ya wavu.
9 Tanzi litamkamata kwenye kisigino;
mtego utamshikilia kwa nguvu.
10 Kitanzi kimefichwa ardhini kwa ajili yake;
mtego uko kwenye njia yake.
11 Vitisho vimemtia hofu kila upande,
na adui zake humwandama kila hatua.
12 Janga linamwonea shauku;
maafa yako tayari kwa ajili yake aangukapo.
13 Nayo yatakula sehemu ya ngozi yake;
mzaliwa wa kwanza wa mauti atakula maungo yake.
14 Atang'olewa kutoka usalama wa hema lake,
na kupelekwa kwa mfalme wa vitisho.
15 Moto utakaa katika hema lake;
moto wa kiberiti utamwagwa juu ya makao yake.
16 Mizizi yake chini itakauka
na matawi yake juu yatanyauka.
17 Kumbukumbu lake litatoweka katika dunia,
wala hatakuwa na jina katika nchi.
18 Ameondolewa nuruni na kusukumiwa gizani,
naye amefukuzwa mbali atoke duniani.
19 Hana mtoto wala mzao miongoni mwa watu wake,
wala aliyenusurika mahali alipoishi.
20 Watu wa magharibi watashangaa yaliyompata;
watu wa mashariki watapatwa na hofu.
21 Hakika ndivyo yalivyo makao ya mtu mwovu;

ndivyo palivyo mahali pake mtu asiyemjua
Mungu.”

# 19

## Hotuba ya sita ya Ayubu

*Ayubu anajibu: Najua Mkombozi wangu yu hai*

1 Ndipo Ayubu akajibu:
2 “Je, mtaendelea kunitesa hadi lini,
na kuniponda kwa maneno yenu?
3 Mara kumi hizi mmenishutumu;
bila aibu mnanishambulia.
4 Kama ni kweli nimepotoka,
kosa langu ninabaki kuhusika nalo
mwenyewe.
5 Kama kweli mngejitukuza wenyewe juu yangu,
na kutumia unyonge wangu dhidi yangu,
6 basi jueni kuwa Mungu amenitendea yaliyo
mabaya,
naye amekokota wavu wake kunizunguka.

7 “Ingawa ninalia, ‘Nimetendewa mabaya!’ sipati
jibu;
ingawa ninaomba msaada, hakuna haki.
8 Yeye ameizuia njia yangu hivyo siwezi kupita;
ameyafunika mapito yangu na giza.
9 Amenivua heshima yangu,
na kuniondolea taji kichwani pangu.
10 Amenibomoa kila upande hadi nimeisha;
ameling’oa tegemeo langu kama mti.
11 Hasira yake imewaka juu yangu;
amenihesabu kuwa miongoni mwa adui
zake.
12 Majeshi yake yananisogelea kwa nguvu;

yamenizingira,
yamepiga kambi kulizunguka hema langu.

13 “Amewatenga ndugu zangu mbali nami;
wale tunaojuana nao wamefarakana nami kabisa.
14 Watu wa jamaa zangu wameenda mbali;
rafiki zangu wamenisahau.
15 Wageni wangu na wajakazi wangu wananiona kama mgeni;
wananitazama kama mgeni.
16 Namwita mtumishi wangu, wala haitiki,
ingawa namwomba kwa kinywa changu mwenyewe.
17 Pumzi ya kinywa changu ni kinyaa kwa mke wangu;
nimekuwa chukizo mno kwa ndugu zangu mwenyewe.
18 Hata watoto wadogo hunidhihaki;
ninapojitokeza, hunifanyia mzaha.
19 Rafiki zangu wa moyoni wote wananichukia kabisa;
wale ninaowapenda wamekuwa kinyume nami.
20 Mimi nimebaki mifupa na ngozi tu;
nimeponea nikiwa karibu kufa.

21 “Nihurumieni, rafiki zangu, kuweni na huruma,
kwa kuwa mkono wa Mungu umenipiga.
22 Kwa nini mnanifuatia kama Mungu afanyavyo?
Hamtosheki kamwe na mwili wangu?

23 “Laiti maneno yangu yangewekwa kwenye kumbukumbu,
laiti kwamba yangeandikwa kwenye kitabu,
24 kwamba yangechorwa kwenye risasi kwa kifaa cha chuma,
au kuyachonga juu ya mwamba milele!
25 Ninajua kwamba Mkombozi* wangu yu hai,
naye kwamba mwishoni atasimama juu ya nchi.
26 Nami baada ya ngozi yangu kuharibiwa,
bado nikiwa na mwili huu nitamwona Mungu;
27 mimi nitamwona kwa macho yangu mwenyewe:
mimi, wala si mwingine.
Tazama jinsi moyo wangu unavyomtamani sana!

28 “Mkisema, ‘Tazama tutakavyomwinda,
maadamu mzizi wa tatizo uko ndani yake,’
29 ninyi wenyewe uogopeni upanga,
kwa kuwa ghadhabu italeta adhabu kwa upanga,
nanyi ndipo mtajua kuwa kuna hukumu.”

# 20

*Sofari anasema: Uovu hupokea malipo ya haki*

1 Ndipo Sofari Mnaamathi akajibu:
2 “Mawazo yanayonisumbua yananisukuma kujibu,
kwa sababu nimehangaika sana.

* **19:25** au *Mtetezi*

3 Ninasikia makaripio ambayo yananivunjia heshima,
nao ufahamu wangu unanisukuma kujibu.

4 “Hakika unajua jinsi ilivyokuwa tangu zamani,
tangu zamani mwanadamu alipowekwa duniani,
5 macheko ya mtu mwovu ni ya muda mfupi,
nayo furaha ya wasiomcha Mungu hudumu kwa kitambo tu.
6 Ingawa kujikweza kwake hufikia mbinguni
na kichwa chake hugusa mawingu,
7 ataangamia milele kama mavi yake mwenyewe.
Wale waliomwona watauliza, ‘Yuko wapi?’
8 Kama ndoto hutoweka, wala hapatikani tena,
amefukuziwa mbali kama maono ya usiku.
9 Jicho lililomwona halitamwona tena;
mahali pake hapatamwona tena.
10 Watoto wake watalipa yote baba yao aliyowadhulumu maskini,
nayo mikono yake itarudisha mali yote aliyonyang’anya watu.
11 Nguvu za ujana zilizoijaza mifupa yake,
zitalala naye mavumbini.

12 “Ingawa uovu ni mtamu kinywani mwake
naye huuficha chini ya ulimi wake,
13 ingawa hawezi kukubali kuuachia uende,
lakini huuweka kinywani mwake.
14 Hata hivyo chakula chake kitakuwa kichungu tumboni mwake,
nacho kitakuwa sumu kali ya nyoka ndani yake.

15 Atatema mali alizozimeza;
Mungu atalifanya tumbo lake kuzitapika.
16 Atanyonya sumu za majoka;
meno ya nyoka mwenye sumu kali yatamuua.
17 Hatafurahia vijito,
mito inayotiririsha asali na siagi.
18 Vile alivyovitaabikia atavirudisha bila kuvila;
hatafurahia faida itokanayo na biashara yake.
19 Kwa kuwa aliwadhulumu maskini na kuwaacha bila kitu;
amenyang'anya kwa nguvu nyumba asizozijenga.

20 "Hakika hatakuwa na amani katika kutamani kwake;
hawezi kujiokoa mwenyewe kwa hazina zake.
21 Hakuna chochote kitakachosalia kwa ajili yake ili ale;
kufanikiwa kwake hakutadumu.
22 Katikati ya wingi wa ustawi wake, dhiki itampata;
taabu itamjia kwa nguvu zote.
23 Atakapokuwa amelijaza tumbo lake,
Mungu ataionesha ghadhabu kali dhidi yake,
na kumnyeshea mapigo juu yake.
24 Ijapokuwa aikimbia silaha ya chuma,
mshale wa shaba utamchoma.
25 Atauchomoa katika mgongo wake,
ncha inayong'aa kutoka ini lake.
Vitisho vitakuja juu yake;
26 giza nene linavizia hazina zake.

Moto usiopepewa na mtu utamteketeza,
na kuangamiza yaliyosalia nyumbani mwake.
27 Mbingu zitaweka wazi hatia yake,
nayo nchi itainuka kinyume chake.
28 Mafuriko yataichukua nyumba yake,
maji yaendayo kasi katika siku ya ghadhabu ya Mungu.
29 Hili ndilo fungu Mungu alilowagawia waovu,
urithi uliowekwa kwa ajili yao na Mungu.”

# 21

## Hotuba ya saba ya Ayubu

*Ayubu anajibu: Waovu mara nyingi huenda bila kuadhibiwa*

1 Ndipo Ayubu akajibu:
2 “Yasikilizeni maneno yangu kwa makini;
hii na iwe faraja mnayonipa mimi.
3 Nivumilieni ninapozungumza,
nami nikishazungumza, endeleeni kunidhihaki.

4 “Je, kwani malalamiko yangu yanaelekezwa kwa mwanadamu?
Kwa nini nisikose subira?
5 Niangalieni mkastaajabu;
mkaweke mkono juu ya vinywa vyenu.
6 Ninapowaza kuhusu hili, ninaogopa,
nao mwili wangu unatetemeka.
7 Kwa nini waovu wanaendelea kuishi,
wakifikia umri wa uzee na kuendelea kuwa na nguvu?
8 Huwaona watoto wao wakithibitika

wakiwa wamewazunguka,
wazao wao mbele za macho yao.
9 Nyumba zao zi salama wala hakuna hofu;
fimbo ya Mungu haiko juu yao.
10 Madume yao ya ng'ombe huvyaza bila kushindwa kamwe;
ng'ombe wao huzaa wala hawaharibu mimba.
11 Huwatoa watoto wao nje kama kundi;
wadogo wao huchezacheza.
12 Huimba nyimbo kwa matari na kwa kinubi,
nao huifurahia sauti ya filimbi.
13 Huitumia miaka yao katika mafanikio
nao hushuka kaburini kwa amani.
14 Lakini humwambia Mungu, 'Tuache sisi!'
Hatuna haja ya kufahamu njia zako.
15 Mwenyezi ni nani hata tumtumikie?
Tutapata faida gani kumwomba?
16 Lakini kufanikiwa kwao hakupo mikononi mwao wenyewe,
hivyo najitenga mbali na ushauri wa waovu.

17 "Lakini ni mara ngapi taa ya waovu huzimwa?
Ni mara ngapi maafa huwajia,
yale yawapatayo ambayo Mungu
huwapangia katika hasira yake?
18 Ni mara ngapi huwa kama majani makavu mbele ya upepo,
kama makapi yachukuliwayo na dhoruba?
19 Imesemekana, 'Mungu huiweka akiba adhabu ya mtu
kwa ajili ya wanawe.'
Mungu na amlipe mtu mwenyewe,

ili apate kulijua!
20 Macho yake mwenyewe na yaone maangamizi yake;
yeye na ainywe ghadhabu ya Mwenyezi.
21 Kwani anajali nini kuhusu jamaa anayoiacha nyuma,
miezi yake aliyopangiwa ifikapo mwisho?

22 “Je, yuko mtu yeyote awezaye kumfundisha Mungu maarifa,
iwapo yeye ndiye ahukumuye hata walio juu ya wote?
23 Mtu mmoja hufa akiwa na nguvu zake kamili,
akiwa salama na mwenye amani,
24 mwili wake ukiwa umenawiri,
nayo mifupa yake ikiwa imejaa mafuta.
25 Mtu mwingine hufa katika uchungu wa nafsi,
akiwa hajafurahia kamwe jambo lolote zuri.
26 Hao wote hulala mavumbini,
nao mabuu huwafunika wote.

27 “Ninayajua kikamilifu yale mnayoyafikiri,
mipango ambayo kwayo mngenitendea mabaya.
28 Mwasema, ‘Iko wapi sasa nyumba ya huyo mtu mkuu,
mahema ambayo watu waovu walikaa?’
29 Je, hamkuwahi kuwauliza hao wanaosafiri?
Je, hamkutafakari taarifa zao:
30 kwamba mtu mwovu huepushwa kutoka siku ya maafa,
kwamba huokolewa kutoka siku ya ghadhabu?

31 Ni nani hulaumu matendo yake mbele ya uso wake?
Ni nani ampatilizaye kwa yale aliyoyatenda?
32 Hupelekwa kaburini,
nao ulinzi ukawekwa kwenye kaburi lake.
33 Udongo ulio bondeni ni mtamu kwake;
watu wote watamfuata,
nao umati wa watu wasiohesabika wamemtangulia.

34 "Hivyo ninyi mnawezaje kunifariji kwa upuzi wenu?
Hakuna kilichosalia cha majibu yenu isipokuwa uongo!"

# 22

## *Elifazi anasema: Uovu wa Ayubu ni mkubwa*

1 Ndipo Elifazi Mtemani akajibu:
2 "Je, mwanadamu aweza kuwa wa faida kwa Mungu?
Je, hata mtu mwenye hekima aweza kumfaidi?
3 Je, Mwenyezi angefurahia nini
kama ungekuwa mwadilifu?
Au je, yeye angepata faida gani
kama njia zako zingekuwa kamilifu?

4 "Je, ni kwa ajili ya utaua wako ndiyo maana anakukemea
na kuleta mashtaka dhidi yako?
5 Je, uovu wako si mkuu?
Dhambi zako si hazina mwisho?
6 Umedai dhamana kwa ndugu zako bila sababu;

umewavua watu nguo zao, ukawaacha uchi.
7 Hukumpa maji aliyechoka,
nawe ulimnyima chakula mwenye njaa,
8 ingawa ulikuwa mtu mwenye uwezo ukimiliki nchi:
mtu uliyeheshimiwa, ukiishi ndani yake.
9 Umewafukuza wajane mikono mitupu
na kuzivunja nguvu za yatima.
10 Ndiyo sababu mitego imekuzunguka pande zote,
hatari ya ghafula inakutia hofu,
11 ndiyo sababu ni giza sana huwezi kuona,
tena ndiyo sababu mafuriko ya maji yamekufunika.

12 “Je, Mungu hayuko katika mbingu za juu?
Juu kuliko nyota zilizo juu sana!
13 Hivyo wewe wasema, ‘Mungu anajua nini?’
Je, yeye huhukumu katika giza kama hilo?
14 Mawingu mazito ni pazia lake, hivyo hatuoni sisi
atembeapo juu ya anga la dunia.
15 Je, utaifuata njia ya zamani,
ambayo watu waovu waliikanyaga?
16 Waliondolewa kabla ya wakati wao,
misingi yao ikachukuliwa na mafuriko.
17 Walimwambia Mungu, ‘Tuache sisi!
Huyo Mwenyezi aweza kutufanyia nini?’
18 Lakini ndiye alizijaza nyumba zao na vitu vizuri,
hivyo ninajitenga mbali na mashauri ya waovu.

19 “Wenye haki wanaona maangamizi yao na kufurahi,
nao wasio na hatia huwadhihaki, wakisema,
20 ‘Hakika adui zetu wameangamizwa,
nao moto umeteketeza mali yao.’

21 “Mjue sana Mungu ili uwe na amani,
ndipo mema yatakapokujia.
22 Uyapokee mafundisho toka kinywani mwake,
na maneno yake uyaweke moyoni mwako.
23 Ukimrudia Mwenyezi, utarudishwa upya:
Ukiuondoa uovu uwe mbali na hema lako,
24 kama dhahabu yako ukiihesabu kama mavumbi,
dhahabu yako ya Ofiri kama miamba ya mabondeni,
25 ndipo Mwenyezi atakuwa dhahabu yako,
naye atakuwa fedha yako iliyo bora.
26 Hakika ndipo utakapojifurahisha kwa Mwenyezi,
nawe utamwinulia Mungu uso wako.
27 Utamwomba yeye, naye atakusikia,
nawe utazitimiza nadhiri zako.
28 Utakusudia jambo nalo litatendeka,
nao mwanga utaangazia njia zako.
29 Watu watakaposhushwa, nawe ukasema, ‘Wainue!’
ndipo atamwokoa aliyevunjika moyo.
30 Atamwokoa hata yule ambaye ana hatia,
ataokolewa kwa sababu ya usafi wa mikono yako.”

# 23
## Hotuba ya nane ya Ayubu

*Ayubu anajibu: Nalalamika kwa uchungu*

1 Ndipo Ayubu akajibu:
2 “Hata leo malalamiko yangu ni ya uchungu;
mkono wake ni mzito juu yangu hata nikiugua.
3 Laiti ningefahamu mahali pa kumwona;
laiti ningeweza kwenda mahali akaapo!
4 Ningeleta kesi yangu mbele zake,
na kukijaza kinywa changu na hoja.
5 Ningejua kwamba angenijibu nini,
na kuelewa lile angeniambia.
6 Je, angenipinga kwa nguvu nyingi?
La, hangenigandamiza.
7 Hapo mtu mwadilifu angeleta kesi yake mbele zake,
nami ningeokolewa milele na mhukumu wangu.

8 “Lakini nikienda mashariki, hayupo;
nikienda magharibi, simpati.
9 Anapokuwa kazini pande za kaskazini, simwoni;
akigeukia kusini, nako simwoni hata kidogo.
10 Lakini anaijua njia niiendeayo;
akiisha kunijaribu, nitatoka kama dhahabu.
11 Nyayo zangu zimefuata hatua zake kwa karibu;
nimeishika njia yake bila kukengeuka.
12 Sijaziacha amri zilizotoka mdomoni mwake;
nimeyathamini maneno ya kinywa chake
kuliko chakula changu cha kila siku.

13 “Lakini yeye husimama peke yake; ni nani awezaye kumpinga?
Yeye hufanya lolote atakalo.
14 Hutimiliza maagizo yake dhidi yangu,
na bado anayo mipango mingi kama hiyo ambayo ameiweka akiba.
15 Hiyo ndiyo sababu ninaingiwa na hofu mbele zake;
nifikiriapo haya yote ninamwogopa.
16 Mungu ameufanya moyo wangu kuzimia;
yeye Mwenyezi amenitia hofu.
17 Hata hivyo sijanyamazishwa na giza,
wala kwa giza nene linalofunika uso wangu.

# 24

*Ayubu anaendelea*

1 “Kwa nini Mwenyezi asiweke nyakati kwa ajili ya hukumu?
Kwa nini wale wamjuao wazitafute siku kama hizo bila mafanikio?
2 Watu husogeza mawe ya mpaka;
huchunga makundi ya wanyama waliyonyang’anya kwa nguvu.
3 Huwanyang’anya yatima punda wao,
na kumchukua rehani fahali wa mjane.
4 Humsukuma mhitaji kutoka njia,
na kuwafanya maskini wote wa nchi kulazimika kujificha.
5 Kama punda-mwitu jangwani,
maskini huzunguka katika kazi zao za kutafuta chakula;
mahali palipo jangwa

huwapa chakula cha watoto wao.
6 Hukusanya chakula mashambani na kuokota masazo
katika mashamba ya mizabibu ya waovu.
7 Kwa kukosa nguo, usiku kucha hukaa uchi;
hawana chochote cha kujifunika baridi.
8 Hutota kwa mvua za mlimani,
nao huikumbatia miamba kwa ajili ya kukosa pa kujisitiri.
9 Mtoto yatima hupokonywa matitini;
mtoto mchanga wa maskini hunyakuliwa kwa ajili ya deni.
10 Kwa kukosa nguo, hutembea uchi;
hubeba miganda ya ngano, lakini huwa na njaa.
11 Hukamua zeituni katika mawe ya kusagia;
hukanyaga mashinikizo, lakini wanaona kiu.
12 Kilio cha huzuni cha wanaokufa kinapaa kutoka mjini,
nazo nafsi za waliojeruhiwa zinalilia msaada.
Lakini Mungu hamlaumu mtu yeyote
kwa kutenda mabaya.

13 “Wako wale wanaoiasi nuru,
wasiofahamu njia zake
wala hawakai katika mapito yake.
14 Mwanga wa mchana unapotoweka, muuaji huinuka,
naye huwaua maskini na mhitaji;
wakati wa usiku hunyemelea kama mwizi.
15 Jicho la mzinzi hungojea wakati wa giza,
naye hufikiri, ‘Hakuna jicho litakaloniona,’

naye huuficha uso wake.
16 Katika giza, huvunja nyumba,
lakini wakati wa mchana hujifungia ndani;
hawataki kufanya lolote nuruni.
17 Kwa wote hawa, giza nene ndiyo asubuhi yao;
hujifanya rafiki na vitisho vya gizani.

18 “Lakini wao ni povu juu ya maji;
sehemu yao juu ya nchi imelaaniwa,
hivyo hakuna hata mmoja
aendaye kwenye shamba la mizabibu.
19 Kama vile joto na hari vinyakuavyo theluji iliyoyeyuka,
ndivyo Kuzimu* kuwanyakuavyo waliotenda dhambi.
20 Tumbo lililowazaa huwasahau,
nao huwa karamu ya mabuu;
watu waovu hawakumbukwi tena,
lakini huvunjika kama mti.
21 Huwafanya mawindo wanawake tasa na wasio na watoto,
nao hawaoneshi huruma kwa wajane.
22 Lakini Mungu huwakokota wenye nguvu kwa uwezo wake;
ingawa wamestawi, hawana hakika ya maisha.
23 Aweza akawaacha wakapumzika wakijihisi salama,
lakini macho yake yanaona njia zao.
24 Kwa kitambo kidogo hutukuka,
hatimaye hutoweka;

* **24:19** Kuzimu kwa Kiebrania ni *Sheol*, yaani *Shimo lisilo na mwisho*

hushushwa na kukusanywa
kama wengine wote;
hukatwa kama masuke ya nafaka.

25 “Kama hili sivyo, ni nani awezaye
kunithibitisha kuwa mwongo,
na kuyafanya maneno yangu
kuwa si kitu?”

# 25

*Bildadi anasema: Mwanadamu awezaje kuwa mwadilifu mbele za Mwenyezi Mungu?*

1 Ndipo Bildadi Mshuhi akajibu:
2 “Mamlaka na kuheshimiwa ni vyake Mungu;
yeye huthibitisha amani katika mbingu juu.
3 Je, majeshi yake yaweza kuhesabika?
Ni nani asiyeangaziwa na nuru yake?
4 Mtu awezaje kuwa mwadilifu mbele za Mungu?
Awezaje mtu aliyezaliwa na mwanamke kuwa safi?
5 Ikiwa hata mwezi sio mwangavu
nazo nyota si safi machoni pake,
6 sembuse mtu ambaye ni funza:
mwanadamu ambaye ni buu tu!”

# 26

## Hotuba ya tisa ya Ayubu

*Ayubu anajibu: Utukufu wa Mwenyezi Mungu hauchunguziki*

1 Kisha Ayubu akajibu:
2 “Tazama jinsi ulivyomsaidia mtu asiye na uwezo!

Jinsi ulivyouokoa mkono ulio dhaifu!
3 Ni shauri gani ulilompa yeye asiye na hekima?
Nayo ni busara gani kubwa uliyoonesha!
4 Ni nani aliyekusaidia kutamka maneno hayo?
Nayo ni roho ya nani iliyosema kutoka kinywani mwako?

5 “Wafu wako katika maumivu makuu,
wale walio chini ya maji,
na wale wanaoishi ndani yake.
6 Mauti* iko wazi mbele za Mungu;
Uharibifu† haukufunikwa.
7 Hutandaza anga la kaskazini mahali patupu;
naye huining’iniza dunia mahali pasipo na kitu.
8 Huyafungia maji kwenye mawingu yake,
hata hivyo mawingu hayapasuki kwa uzito wake.
9 Huufunika uso wa mwezi mpevu,
akitandaza mawingu juu yake.
10 Amechora mstari wa upeo juu ya maji,
ameweka mpaka wa nuru na giza.
11 Nguzo za mbingu nazo zatetemeka,
zinatishika anapozikemea.
12 Kwa nguvu zake aliisukasuka bahari;
kwa hekima yake alimkata Rahabu‡ vipande vipande.
13 Aliisafisha anga kwa pumzi yake;

---

* **26:6** yaani *Kuzimu*; Kiebrania ni *Sheol* † **26:6** kwa Kiebrania ni *Abadon* ‡ **26:12** Rahabu hapa ni fumbo la kumaanisha *Lewiathani*, mnyama mkubwa wa baharini mwenye magamba anayefanana na joka kubwa, mwenye umbo la kutisha, asiyeweza kuvuliwa.

kwa mkono wake alimchoma joka aendaye mbio.
14 Haya ni mambo madogo tu katika matendo yake;
tazama jinsi ulivyo mdogo mnong'ono tunaousikia kumhusu!
Ni nani basi awezaye kuelewa
ngurumo za nguvu zake?"

# 27

### *Neno la mwisho la Ayubu kwa rafiki zake*

1 Ndipo Ayubu akaendelea na hoja yake, akasema:
2 "Hakika kama Mungu aishivyo, aliyeninyima haki yangu,
Mwenyezi ambaye amenifanya
nionje uchungu wa nafsi,
3 kwa muda wote nitakaokuwa na uhai ndani yangu,
nayo pumzi ya Mungu ikiwa puani mwangu,
4 midomo yangu haitanena uovu,
wala ulimi wangu hautatamka udanganyifu.
5 Sitakubaliana nanyi kabisa kuwa mko sahihi;
hadi nife, sitakana uadilifu wangu.
6 Nitadumisha haki yangu wala sitaiacha;
dhamiri yangu haitanisuta muda wote ninaoishi.

7 "Watesi wangu wawe kama waovu,
nao adui zangu wawe kama wasio haki!
8 Kwa maana mtu asiyemcha Mungu
analo tegemeo gani anapokatiliwa mbali,
Mungu anapouondoa uhai wake?

9 Je, Mungu husikiliza kilio chake,
shida zimjiapo?
10 Je, anaweza kumfurahia Mwenyezi?
Je, atamwita Mungu nyakati zote?

11 “Nitawafundisha kuhusu uweza wa Mungu;
njia za Mwenyezi sitazificha.
12 Ninyi nyote mmeona hili wenyewe.
Ni ya nini basi mazungumzo haya yasiyo na maana?

13 “Hili ndilo fungu ambalo Mungu humpa mtu mwovu,
urithi ule mtu mdhalimu anapokea kutoka kwa Mwenyezi:
14 Hata watoto wake wawe wengi kiasi gani,
fungu lao ni kuuawa kwa upanga;
wazao wake hawatakuwa kamwe
na chakula cha kuwatosha.
15 Tauni itawazika wale watakaonusurika miongoni mwao,
nao wajane wao hawatawaombolezea.
16 Ajapokusanya fedha nyingi kama mavumbi,
na mavazi kama malundo ya udongo wa mfinyanzi,
17 yale yote mtu mwovu aliyojiwekea akiba,
mwenye haki atayavaa,
naye asiye na hatia
ataigawanya fedha yake.
18 Nyumba aijengayo ni kama utando wa buibui,
kama kibanda alichotengeneza mlinzi.
19 Yeye hulala akiwa tajiri, lakini ndiyo mara ya mwisho;
afunguapo macho yake, yote yametoweka.

20 Vitisho humjia kama mafuriko;
dhoruba humkumba ghafula usiku.
21 Upepo mkali wa mashariki humchukua, naye hutoweka;
humzoa kutoka mahali pake.
22 Humvurumisha bila huruma,
huku akikimbia kasi kukwepa nguvu zake.
23 Upepo humpigia makofi kwa dharau,
na kumfukuza atoke mahali pake.”

# 28

*Mapumziko: Hekima inakopatikana*

1 Kuna machimbo ya fedha,
na mahali dhahabu inaposafishwa.
2 Chuma hupatikana ardhini,
nayo shaba huyeyushwa kutoka mawe ya madini.
3 Mwanadamu hukomesha giza;
huyatafuta hadi sehemu iliyo mbali,
kwa ajili ya kuchimbua mawe yenye madini
katika giza jeusi sana.
4 Huchimba shimo jembamba mbali na makao ya watu,
mahali paliposahaulika na nyayo za wanadamu;
mbali na wanadamu huning’inia na kubembea.
5 Ardhi, ambako chakula hutoka,
chini hugeuzwa kwa moto;
6 yakuti samawi hutoka katika miamba yake,
nalo vumbi lake lina vipande vya dhahabu.
7 Hakuna ndege awindaye aijuaye njia ile iliyofichika,

wala hakuna jicho la mwewe lililoiona.
8 Wanyama wa porini wanaotamba hawajawahi kupakanyaga,
wala simba azungukaye huko.
9 Mikono ya mwanadamu hushambulia miamba ya gumegume,
na kuiacha wazi mizizi ya milima.
10 Hutoboa shimo refu la kupenya chini kwa chini kwenye miamba;
macho yake huona hazina zake zote.
11 Hutafuta vyanzo vya mito
na kuvileta vitu vilivyofichika katika nuru.

12 Lakini hekima inaweza kupatikana wapi?
Ufahamu unakaa wapi?
13 Mwanadamu hatambui thamani yake;
haiwezi kupatikana katika nchi ya walio hai.
14 Kilindi husema, “Haiko ndani yangu”;
bahari nayo husema, “Haiko pamoja nami.”
15 Haiwezi kununuliwa kwa dhahabu safi kuliko zote,
wala thamani yake haiwezi kupimwa kwa fedha.
16 Haiwezi kununuliwa kwa dhahabu ya Ofiri,
kwa shohamu ya thamani kubwa au yakuti samawi ya thamani kubwa.
17 Dhahabu wala mawe maangavu haviwezi kulinganishwa nayo,
wala haiwezi hubadilishwa kwa vito vya dhahabu.
18 Marijani na yaspi hazistahili kutajwa;
thamani ya hekima ni zaidi ya akiki nyekundu.

19 Yakuti manjano ipatikanayo Kushi haiwezi kulinganishwa nayo,
wala haiwezi kununuliwa kwa dhahabu safi.

20 Ni wapi basi hekima itokako?
Ufahamu hukaa wapi?
21 Imefichika machoni pa kila kitu kilicho hai,
imesitiriwa hata kwa ndege wa angani.
22 Uharibifu na Mauti husema,
“Ni uvumi wake tu uliotufikia masikioni mwetu.”
23 Mungu anaifahamu njia ya kuiendea hekima
na ndiye peke yake anayefahamu inakokaa,
24 kwa maana yeye huitazama miisho ya dunia
na huona kila kitu chini ya mbingu.
25 Alipoufanyia upepo nguvu zake
na kuyapima maji,
26 alipofanya maagizo kwa ajili ya mvua
na njia ya mwali wa radi,
27 ndipo alipoitazama hekima na kuikadiria thamani yake,
akaithibitisha na kuihakikisha.
28 Naye Mungu akamwambia mwanadamu,
“Kumcha Bwana: hiyo ndiyo hekima,
nako kujitenga na uovu ndio ufahamu.”

# 29

*Ayubu amaliza utetezi wake*

1 Ayubu akaendelea na hoja yake, akasema:
2 “Tazama jinsi ninavyoitamani miezi iliyopita,
zile siku ambazo Mungu alikuwa akinilinda,
3 wakati taa yake ilinimulika kichwani,

na kwa mwanga wa Mungu nikapita katikati ya giza!
4 Natamani siku zile nilizokuwa katika ustawi wangu,
urafiki wa Mungu wa ndani ulipoibariki nyumba yangu,
5 wakati Mwenyezi bado alikuwa pamoja nami,
nao watoto wangu wakawa wamenizunguka,
6 wakati njia yangu ilikuwa imenyeshewa siagi,
nao mwamba ukanimiminia vijito vya mafuta ya zeituni.

7 “Wakati nilienda kwenye lango la mji
na kuketi katika kiwanja,
8 vijana waliniona, wakakaa kando,
nao wazee walioketi, wakasimama;
9 wakuu wakaacha kuzungumza,
na kuziba vinywa vyao kwa mikono yao;
10 wenye vyeo wakanyamazishwa,
nazo ndimi zao zikagandamana na makaakaa ya vinywa vyao.
11 Yeyote aliyenisikia alinena mema juu yangu,
nao walioniona walinisifu,
12 kwa sababu nilimwokoa maskini aliyeomba msaada,
naye yatima aliyekuwa hana wa kumsaidia.
13 Mtu aliyekuwa karibu kufa alinibariki,
nami niliufanya moyo wa mjane kuimba.
14 Niliivaa haki kama vazi langu;
uadilifu ulikuwa joho langu na kilemba changu.
15 Nilikuwa macho ya kipofu

na miguu kwa kiwete.
16 Nilikuwa baba kwa mhitaji;
nilimtetea mgeni.
17 Niliyavunja meno makali ya waovu,
na kuwapokonya wahanga kwenye meno yao.

18 “Nikafikiri, ‘Nitafia katika nyumba yangu mwenyewe,
nazo siku zangu zitakuwa nyingi kama chembechembe za mchanga.
19 Mizizi yangu itafika hata kwenye maji,
nao umande utakaa juu ya matawi yangu usiku kucha.
20 Utukufu wangu utabakia kuwa mpya ndani yangu,
upinde wangu daima utaendelea kuwa mpya mkononi mwangu.’

21 “Watu walinisikiliza kwa tumaini,
wakingojea ushauri wangu kwa utulivu.
22 Baada ya mimi kuzungumza, hawakusema zaidi;
maneno yangu yaliingia masikioni mwao kwa makini.
23 Waliningojea kama manyunyu ya mvua
na kuyapokea maneno yangu
kama ardhi inyonyavyo mvua ya vuli.
24 Walipokata tamaa niliwaonesha uso wa furaha;
nuru ya uso wangu ilikuwa ya thamani kwao.
25 Niliwachagulia njia na kukaa kama mkuu wao;

niliishi kama mfalme katikati ya majeshi yake;
nikawa kama yeye anayewafariji waombolezaji.

# 30

*Ayubu anaendelea*

1 “Lakini sasa watu wadogo kwa umri kuliko mimi wananidhihaki,
watu ambao baba zao ningekataa kwa dharau
kuwaweka pamoja na mbwa wangu wa kulinda kondoo.
2 Nguvu za mikono yao zingekuwa na faida gani kwangu,
kwa kuwa nguvu zao zilikuwa zimewaishia?
3 Wakiwa wamekonda kutokana na kupungukiwa na kwa njaa,
walizurura usiku katika nchi kame iliyo ukiwa.
4 Katika vichaka walikusanya mimea ya chumvi,
nacho chakula chao kilikuwa mizizi ya mti wa mfagio.
5 Walifukuzwa mbali na watu wao,
wakipigiwa kelele kama wezi.
6 Walilazimika kuishi katika mikondo ya vijito vilivyokauka,
kwenye majabali na mahandaki.
7 Kwenye vichaka walilia kama punda,
na walijisongasonga pamoja kwenye vichaka.
8 Wao ni watoto wa wapumbavu wenye asili ya ubaya,
waliofukuzwa watoke katika nchi.

9 “Nao sasa wana wao wananidhihaki katika nyimbo;
nimekuwa kitu cha dhihaka kwao.
10 Wananichukia sana na kujitenga nami,
wala hawasiti kunitemea mate usoni.
11 Sasa kwa kuwa Mungu ameilegeza kamba ya upinde wangu na kunitesa,
wamekuwa huru kunitendea wanavyopenda.
12 Kuume kwangu kundi linashambulia;
wao huitegea miguu yangu tanzi,
na kunizingira.
13 Huizuia njia yangu,
nao hufanikiwa katika kuniletea maafa,
nami sina yeyote wa kunisaidia.
14 Wananijia kama watu wapitao katika ufa mpana;
katikati ya magofu huja na kunishambulia.
15 Vitisho vimenifunika;
heshima yangu imetoweshwa kama kwa upepo,
salama yangu imetoweka kama wingu.

16 “Sasa maisha yangu yamefikia mwisho;
siku za mateso zimenikamata.
17 Usiku mifupa yangu inachoma;
maumivu yanayonitafuna hayatulii kamwe.
18 Kwa uwezo wake mkuu Mungu huwa kwangu kama nguo;
hushikamana nami kama ukosi wa vazi langu.
19 Yeye amenitupa kwenye matope,
nami nimekuwa kama mavumbi na majivu.

20 “Ee Mwenyezi Mungu, ninakulilia wewe lakini hunijibu;
ninasimama, nawe unanitazama tu.
21 Wewe unanigeukia bila huruma;
unanishambulia kwa nguvu za mkono wako.
22 Unaninyakua na kunipeperusha kwa upepo;
umenirusharusha kwenye dhoruba.
23 Ninajua utanileta hadi kifoni,
mahali wenye uhai wote wamewekewa.

24 “Hakika hakuna mtu anayemshambulia mhitaji
anapoomba msaada katika shida yake.
25 Je, sikulia kwa ajili ya wale waliokuwa katika taabu?
Je, nafsi yangu haikusononeka kwa ajili ya maskini?
26 Lakini nilipotazamia mema, mabaya yalinijia;
nilipotafuta nuru, ndipo giza lilipokuja.
27 Kusukwasukwa ndani yangu kamwe hakutulii;
siku za mateso zinanikabili.
28 Ninazunguka nikiwa nimeungua, lakini si kwa jua;
ninasimama katika kusanyiko nikiomba msaada.
29 Nimekuwa ndugu wa mbweha,
rafiki wa mabundi.
30 Ngozi yangu imekuwa nyeusi nayo inachunika;
mifupa yangu inaungua kwa homa.
31 Kinubi changu kimegeuka kuwa maombolezo,
nayo filimbi yangu imekuwa sauti ya kilio.

# 31

*Ayubu anakamilisha maneno yake*

1 “Nimefanya agano na macho yangu
yasimtazame msichana kwa kumtamani.
2 Kwa kuwa fungu la mwanadamu ni lipi kutoka kwa Mungu juu,
urithi wake kutoka juu kwa Mwenyezi?
3 Je, si uharibifu kwa watu waovu,
maangamizi kwa wale watendao mabaya?
4 Je, yeye hazioni njia zangu
na kuihesabu kila hatua yangu?

5 “Kama nimeishi katika uongo
au mguu wangu umekimbilia udanganyifu,
6 Mungu na anipime katika mizani za uaminifu,
naye atajua kwamba sina hatia:
7 kama hatua zangu zimepotoka kutoka njia,
kama moyo wangu umeongozwa na macho yangu,
au kama mikono yangu imetiwa unajisi,
8 basi wengine na wale nilichokipanda,
nayo yale yote niliyootesha na yang’olewe.

9 “Kama moyo wangu umeshawishiwa na mwanamke,
au kama nimevizia mlangoni mwa jirani yangu,
10 basi mke wangu na asage nafaka ya mwanaume mwingine,
nao wanaume wengine walale naye.
11 Kwa kuwa hilo lingekuwa aibu,
naam, dhambi ya kuhukumiwa.

12 Ni moto uwakao kwa Uharibifu*;
ungekuwa umeng'oa mavuno yangu.

13 "Kama ningewanyima haki watumishi wangu
wanaume au vijakazi wangu,
walipokuwa na manung'uniko dhidi yangu,
14 nitafanya nini Mungu atakaponikabili?
Nitamjibu nini nitakapoitwa kujitetea?
15 Je, yeye aliyeniumba tumboni mwa mama yangu,
siye aliyewaumba?
Je, si ni yeye huyo mmoja aliyetuumba sote
ndani ya mama zetu?

16 "Ikiwa nimewanyima maskini haja zao,
au kuyaacha macho ya wajane yadhoofike,
17 kama nimekula chakula changu mwenyewe,
bila kuwashirikisha yatima;
18 lakini tangu ujana wangu nimemlea yatima
kama ambavyo baba angefanya,
nami tangu kuzaliwa kwangu nimewaongoza wajane:
19 kama nilimwona yeyote akiteseka kwa kukosa nguo,
au mtu mhitaji asiye na mavazi,
20 ambaye wala moyo wake haukunibariki
kwa kumpatia joto kwa mavazi ya manyoya ya kondoo wangu,
21 na kama nimeinua mkono wangu dhidi ya yatima,
nikijua kuwa nina ushawishi mahakamani,

* **31:12** Kwa Kiebrania ni *Abadon* (Ayubu 26:6; Mithali 15:11).

22 basi mkono wangu na unyofoke toka begani mwangu,
nao na uvunjike kutoka kiungio chake.
23 Kwa kuwa niliogopa uharibifu kutoka kwa Mungu,
nami kwa kuuogopa utukufu wake sikuweza kufanya mambo kama hayo.

24 “Kama nimeweka tumaini langu kwenye dhahabu,
au kuiambia dhahabu safi, ‘Wewe ndiwe salama yangu,’
25 kama nimefurahia wingi wa utajiri wangu,
ustawi ambao mikono yangu ilikuwa imepata,
26 kama nimelitazama jua katika kung’aa kwake
au mwezi ukienda kwa fahari yake,
27 hivyo moyo wangu kushawishiwa kwa siri,
au kubusu mkono wangu kwa kuviheshimu,
28 basi hiyo pia ingekuwa dhambi ya kuhukumiwa,
kwa kuwa ningekuwa si mwaminifu kwa Mungu aishiye juu sana.

29 “Kama nimeshangilia msiba wa adui yangu,
au kutazama kwa furaha taabu iliyomjia,
30 lakini sikuruhusu kinywa changu kufanya dhambi
kwa kuomba laana dhidi ya maisha yake;
31 kama watu wa nyumbani mwangu kamwe hawakusema,
‘Ni nani ambaye hajashibishwa na nyama ya Ayubu?’

32 Lakini hakuna mgeni aliyelala njiani,
kwa maana mlango wangu ulikuwa wazi kwa msafiri;
33 kama nimeifunika dhambi yangu kama wanadamu wengine wafanyavyo,
kwa kuficha hatia yangu moyoni mwangu,
34 kwa sababu ya kuogopa umati wa watu,
na hivyo kuwa na hofu ya kudharauliwa na jamaa,
nikakaa kimya, nisitoke nje ya mlango.

35 (“Laiti angekuwepo mtu wa kunisikia!
Tazama sasa ninatia sahihi kwenye utetezi wangu:
Mwenyezi na anijibu;
mshtaki wangu na aweke mashtaka yake kwenye maandishi.
36 Hakika ningeyavaa begani mwangu,
ningeyavaa kama taji.
37 Ningempa hesabu ya kila hatua yangu,
ningemwendea kama mwana wa mfalme.)

38 “Kama nchi yangu inalia dhidi yangu,
na mifereji yake yote imelowana kwa machozi,
39 kama nimekula mazao yake bila malipo,
au kuvunja mioyo ya wapangaji wake,
40 basi miiba na iote badala ya ngano,
na magugu badala ya shayiri.”
Mwisho wa maneno ya Ayubu.

# Sehemu ya tatu: Mazungumzo ya Elihu

# 32

*(Ayubu 32–37)*

## *Elihu awakemea rafiki zake Ayubu*

1 Basi watu hawa watatu wakaacha kumjibu
Ayubu, kwa kuwa alikuwa mwadilifu machoni
pake mwenyewe.
2 Lakini Elihu mwana wa Barakeli, wa ka-
bila la Buzi wa jamaa ya Ramu, akamkasirikia
sana Ayubu, kwa sababu ya kujihesabia haki
mwenyewe badala ya Mungu.
3 Pia aliwakasirikia hao rafiki watatu wa
Ayubu, kwa sababu hawakuweza kupata njia ya
kuthibitisha ya kuwa hayo maneno ya Ayubu
hayakuwa ya kweli, nao bado walikuwa wamem-
laumu.
4 Basi Elihu alikuwa amesubiri kwanza
waongee na Ayubu, kwa sababu walikuwa na
umri mkubwa kuliko yeye.
5 Lakini alipoona watu hao watatu hawakuwa
na kitu zaidi cha kusema, hasira yake ikaamka.
6 Basi Elihu mwana wa Barakeli wa kabila la
Buzi akasema:
“Mimi ni mdogo kwa umri,
nanyi ni wazee;
ndiyo sababu niliogopa,
sikuthubutu kuwaambia kile ninachojua.
7 Nilifikiri, ‘Yafaa umri useme,
nao wingi wa miaka ungefundisha hekima.’
8 Lakini ni Roho iliyo ndani ya mwanadamu,
pumzi ya Mwenyezi, ndiyo impayo ufahamu.
9 Sio wazee peke yao walio na hekima,
sio wenye umri mkubwa peke yao wanaofa-
hamu lililo sawa.

10 “Kwa hiyo nasema: Nisikilizeni;
mimi nami nitawaambia ninalolijua.
11 Nilingojea mlipokuwa mnaongea,
nilizisikiliza hoja zenu;
mlipokuwa mkitafuta maneno ya kusema,
12 niliwasikiliza kwa makini.
Lakini hakuna hata mmoja wenu
aliyethibitisha kwamba Ayubu amekosa;
hakuna hata mmoja wenu
aliyeweza kujibu hoja zake.
13 Msiseme, ‘Tumepata hekima;
Mungu na amthibitishe kuwa mwongo,
wala si mwanadamu.’
14 Lakini Ayubu hajayapanga maneno yake dhidi yangu,
nami sitamjibu kwa kutumia hoja zenu.

15 “Wametiwa hofu na hawana la zaidi la kusema;
maneno yamewaishia.
16 Je, ningoje sasa kwa sababu wamekuwa kimya,
kwa vile sasa wanasimama bila kuwa na la kujibu?
17 Mimi nami nitakuwa na la kusema;
mimi nami nitasema lile nilijualo.
18 Kwa kuwa nimejawa na maneno,
nayo Roho iliyo ndani yangu inanisukuma;
19 ndani yangu niko kama chupa iliyojazwa divai,
kama kiriba kipya cha divai kilicho karibu kupasuka.
20 Ni lazima niseme ili niweze kutulia;
ni lazima nifumbue midomo yangu nipate kujibu.
21 Sitampendelea mtu yeyote,

wala sitajipendekeza kwa mtu yeyote;
22 kwa kuwa kama ningekuwa stadi wa kujipendekeza,
Muumba wangu angeniondolea mbali kwa upesi.

# 33

*Elihu amkemea Ayubu*

1 “Lakini Ayubu, sasa sikiliza maneno yangu;
zingatia kila kitu nitakachosema.
2 Karibu nitafungua kinywa changu;
maneno yangu yapo katika ncha ya ulimi wangu.
3 Maneno yangu yanatoka katika moyo mnyofu;
midomo yangu hunena kwa uaminifu yale niyajuayo.
4 Roho wa Mungu ameniumba;
pumzi ya Mwenyezi hunipa uhai.
5 Unijibu basi, kama unaweza;
jiandae kunikabili mimi.
6 Mimi ni kama wewe mbele za Mungu;
mimi pia nimetolewa kwenye udongo.
7 Huna sababu ya kuniogopa,
wala mkono wangu haupaswi kukulemea.

8 “Lakini umesema nikiwa ninakusikia,
nami nilisikia maneno yenyewe:
9 ‘Mimi ni safi na sina dhambi;
mimi ni safi na sina hatia.
10 Lakini bado Mungu amepata dosari kwangu,
naye ananiona kama adui yake.
11 Ananifunga miguu kwa pingu,

tena anaziangalia njia zangu zote kwa karibu.’

12 “Lakini mimi ninakuambia,
katika jambo hili wewe una makosa,
kwa maana Mungu ni mkuu
kuliko mwanadamu.
13 Kwa nini unamlalamikia
kwamba yeye hamjibu mwanadamu?
14 Kwa kuwa Mungu husema,
wakati huu kwa njia moja,
au wakati mwingine kwa njia nyingine,
ingawa mwanadamu anaweza asielewe.
15 Mungu husema na mwanadamu katika ndoto,
katika maono ya usiku,
wakati usingizi mzito uwaangukiapo
wanadamu wasinziapo vitandani mwao,
16 anaweza akasemea masikioni mwao,
na kuwatia hofu kwa maonyo,
17 ili kumgeuza mtu kutoka kutenda mabaya
na kumwepusha na kiburi,
18 kuiokoa nafsi yake na shimo,
uhai wake usiangamizwe kwa upanga.
19 Mtu anaweza kutiwa adabu kwa maumivu kitandani mwake,
kwa dhiki za mfululizo katika mifupa yake,
20 kiasi kwamba maisha yake yenyewe yanakataa chakula
nayo nafsi yake ikakichukia kabisa hata chakula kizuri.
21 Nyama ya mwili wake huisha kwa kukonda,
nayo mifupa yake ambayo mwanzoni ilikuwa imefichika,
sasa inatokeza nje.

22 Nafsi yake inakaribia kaburi,
nao uhai wake karibu na wajumbe wa kifo.

23 “Kama bado kuna malaika upande wake
kama mtetezi, mmoja miongoni mwa elfu,
wa kumwambia mwanadamu lililo jema kwake,
24 kumwonea huruma na kusema,
‘Mwokoe asije akatumbukia shimoni;
nimepata ukombozi kwa ajili yake’:
25 ndipo nyama ya mwili wake hufanywa mpya kama ya mtoto;
hurudishwa upya kama siku za ujana wake.
26 Humwomba Mungu, akapata kibali kwake,
huuona uso wa Mungu na kushangilia kwa furaha;
Mungu humrudisha katika hali yake ya uadilifu.
27 Ndipo huja mbele za watu na kusema,
‘Nilitenda dhambi na kupotosha kilichokuwa haki,
lakini sikuadhibiwa kama nilivyostahili.
28 Alinikomboa nafsi yangu nisitumbukie shimoni,
nami nitaishi ili kuufurahia mwanga.’

29 “Mungu hufanya haya yote kwa mwanadamu;
mara mbili hata mara tatu,
30 ili aigeuze nafsi yake toka shimoni,
ili nuru ya uzima imwangazie.

31 “Ayubu, zingatia, nisikilize mimi;
nyamaza, nami nitanena.

32 Kama unalo lolote la kusema, unijibu;
sema, kwa maana ninataka uonekane huna hatia.
33 Lakini kama huna la kusema, basi nisikilize mimi;
nyamaza, nami nitakufundisha hekima."

# 34

## *Elihu atangaza haki ya Mwenyezi Mungu*

1 Kisha Elihu akasema:
2 "Sikieni maneno yangu, enyi watu wenye hekima;
nisikilizeni mimi, ninyi watu wenye maarifa.
3 Kwa kuwa sikio huyajaribu maneno
kama vile ulimi uonjavyo chakula.
4 Tujichagulie wenyewe yaliyo sawa,
nasi tujifunze pamoja yaliyo mema.

5 "Ayubu anasema, 'Mimi sina hatia,
lakini Mungu ameninyima haki yangu.
6 Ingawa niko sawa,
ninaonekana mwongo;
nami ingawa sina kosa,
kidonda changu hakiponi.'
7 Ni mtu gani aliye kama Ayubu,
anywaye dharau kama maji?
8 Hushirikiana na watenda maovu,
na kuchangamana na watu waovu.
9 Kwa kuwa anasema, 'Haimfaidi mwanadamu kitu chochote
anapojitahidi kumpendeza Mungu.'

10 “Hivyo nisikilizeni mimi, ninyi watu wenye ufahamu.
Kamwe Mungu hatendi uovu,
Mwenyezi hafanyi kosa.
11 Humlipa mwanadamu kwa ajili ya lile alilotenda;
huleta juu yake kile ambacho matendo yake yanastahili.
12 Ni jambo lisilofikirika kwamba Mungu angefanya makosa,
kwamba Mwenyezi angepotosha hukumu.
13 Je, ni nani aliyemtawaza juu ya dunia?
Ni nani aliyemweka kuwa mwangalizi wa ulimwengu wote?
14 Kama lilikuwa kusudi la Mungu,
naye akaiondoa Roho yake na pumzi yake,
15 wanadamu wote wangeangamia kwa pamoja,
na mtu angerudi mavumbini.

16 “Kama ninyi mnaufahamu, sikieni hili;
sikilizeni hili nisemalo.
17 Je, yeye aichukiaye haki aweza kutawala?
Je, utamhukumu mwenye haki,
yeye Aliye na Nguvu Zote?
18 Je, si ni yeye awaambiaye wafalme, ‘Ninyi hamfai kitu,’
nao watu mashuhuri, ‘Ninyi ni waovu,’
19 yeye asiyependelea wakuu,
wala haoneshi upendeleo kwa matajiri kuliko maskini,
kwa kuwa wote ni kazi ya mikono yake?
20 Wanakufa ghafula, usiku wa manane;
watu wanatikiswa nao hupita;

wenye nguvu huondolewa
bila mkono wa mwanadamu.

21 “Macho yake yanazitazama njia za wanadamu;
anaona kila hatua yao.
22 Hakuna mahali penye giza nene, wala uvuli mkubwa,
ambapo watenda maovu wanaweza kujificha.
23 Mungu hana haja ya kumchunguza mtu sana,
ili apate kuja mbele zake kwa hukumu.
24 Bila kuuliza huwapondaponda wenye nguvu nyingi
na kuwaweka wengine mahali pao.
25 Kwa sababu huyaangalia matendo yao yote,
huwaondoa usiku, nao wakaangamia.
26 Anawaadhibu kwa ajili ya uovu wao
mahali ambapo kila mmoja ataweza kuwaona,
27 kwa sababu wameacha kumfuata Mungu,
nao hawakuiheshimu njia yake hata moja.
28 Wamesababisha kilio cha maskini kifike mbele zake,
hivyo akasikia kilio cha wahitaji.
29 Lakini akikaa kimya,
ni nani awezaye kumhukumu?
Akiuficha uso wake,
ni nani awezaye kumwona?
Ikiwa ni taifa au mtu mmoja, kwake ni sawa,
30 ili kumzuia mtu mwovu kutawala,
au wale ambao huwategea watu mitego.

31 “Kama mwanadamu akimwambia Mungu,

‘Nimekosa lakini sitatenda dhambi tena.
32 Nifundishe nisichoweza kuona;
kama nimekukosea, sitafanya hivyo tena.’
33 Je basi, Mungu atakulipa kwa masharti yako,
wakati wewe umekataa kutubu?
Yakupasa wewe uamue, wala si mimi;
sasa niambie lile ulijualo.

34 “Watu wenye ufahamu husema,
wenye hekima wanaonisikia huniambia,
35 ‘Ayubu huongea bila maarifa;
maneno yake hayana busara.’
36 Laiti Ayubu angejaribiwa hadi mwisho,
kwa sababu anajibu kama mtu mwovu!
37 Kwenye dhambi yake huongeza uasi;
kwa dharau hupiga makofi miongoni mwetu,
na kuzidisha maneno yake dhidi ya Mungu.”

# 35

*Elihu alaumu mtu kujiona kuwa mwenye haki*

1 Ndipo Elihu akasema:
2 “Je, unadhani hili ni haki?
Wewe unasema, ‘Nina haki mbele za Mungu.’
3 Bado unamuuliza, ‘Ni faida gani nimepata,
na imenifaidi nini kwa kutokutenda dhambi?’

4 “Ningependa nikujibu wewe
na rafiki zako walio nawe.
5 Tazama juu mbinguni ukaone;
yaangalie mawingu yaliyo juu sana juu yako.
6 Je, ukitenda dhambi, inamdhuruje Mungu?
Kama dhambi zako zikiwa nyingi,

hilo linamfanyia nini Mungu?
7 Kama wewe ni mwadilifu, unampa nini,
au yeye anapokea nini mkononi kwako?
8 Uovu wako unamdhuru tu mtu mwingine kama wewe,
nayo haki yako inawafaa wanadamu tu.

9 “Wanadamu hulia kwa kulemewa na mateso;
huomba msaada kutoka mkono wenye nguvu.
10 Lakini hakuna asemaye, ‘Yuko wapi Mungu Muumba wangu,
yeye anifanyaye niimbe usiku,
11 yeye atufundishaye sisi zaidi ya wanyama wa nchi,
na kutufanya wenye hekima kuliko ndege wa angani?’
12 Yeye hajibu wakati watu waliapo
kwa sababu ya kiburi cha watu waovu.
13 Naam, Mungu hasikilizi maombi yao ya ubatili;
Mwenyezi hayazingatii.
14 Si zaidi sana kwamba hatakusikiliza
wewe usemapo humwoni,
tena kwamba kesi yako iko mbele zake
na wewe lazima umngojee,
15 pia zaidi, kwamba hasira yake kamwe haiadhibu
wala haangalii uovu hata kidogo?
16 Hivyo Ayubu hufumbua kinywa chake kwa maneno yasiyo na maana;
anaongea maneno mengi bila maarifa.”

# 36

## *Elihu atukuza wema wa Mwenyezi Mungu*

1 Elihu akaendelea kusema:
2 "Nivumilie kidogo zaidi nami nitakuonesha
kwamba yako mengi zaidi ya kusemwa kwa ajili ya Mungu.
3 Ninayapata maarifa yangu kutoka mbali,
nami nitamhesabia haki Muumba wangu.
4 Uwe na hakika kwamba maneno yangu si ya uongo;
mmoja aliye mkamilifu katika maarifa yuko pamoja na wewe.

5 "Mungu ni mwenye nguvu, lakini hamdharau mwanadamu;
ni mwenye nguvu, naye ni thabiti katika kusudi lake.
6 Hawaachi waovu waendelee kuishi,
bali huwapa walioteswa haki yao.
7 Yeye haondoi macho yake kwa wenye haki;
huwaketisha penye viti vya utawala pamoja na wafalme,
na kuwatukuza milele.
8 Lakini ikiwa watu wamefungwa kwenye minyororo,
wakiwa wameshikiliwa na kamba za mateso,
9 huwaonesha yale waliyoyatenda,
kwamba wametenda dhambi kwa majivuno.
10 Huwafanya wao kusikia maonyo,
na huwaagiza kutubu uovu wao.
11 Wakitii na kumtumikia,
wataishi siku zao zilizobaki katika mafanikio,
na miaka yao katika utoshelevu.

12 Lakini wasiposikiliza,
wataangamia kwa upanga,
nao watakufa pasipo maarifa.

13 “Wasiomcha Mungu moyoni mwao huficha chuki;
hata anapowafunga, hawamwombi msaada.
14 Wanakufa wangali vijana,
miongoni mwa mahanithi wa mahali pa ibada za sanamu.
15 Bali wao wanaoteseka huwaokoa katika mateso yao,
na kuzungumza nao katika dhiki zao.

16 “Yeye anakubembeleza utoke katika mataya ya dhiki,
ili kukuweka mahali palipo na nafasi mbali na kizuizi,
hadi kwenye meza yako ya faraja iliyojaa vyakula vizuri.
17 Lakini sasa umelemewa na hukumu kwa ajili ya uovu;
hukumu na haki vimekukamata.
18 Uwe mwangalifu ili yeyote asikushawishi kwa utajiri;
usipotoshwe kwa fungu kubwa la rushwa.
19 Je, utajiri wako hata nguvu zako nyingi
vinaweza kukusaidia usiingie kwenye dhiki?
20 Usiutamani usiku uje,
ili uwaburute watu mbali na nyumba zao.
21 Jihadhari usigeukie uovu,
ambao unaupenda zaidi ya mateso.

22 “Mungu ametukuzwa katika nguvu zake.
Ni nani aliye mwalimu kama yeye?
23 Ni nani aliyemwelekeza katika njia zake,
au kumwambia, ‘Wewe umetenda yasiyo sawa’?
24 Kumbuka kuzitukuza kazi zake,
ambazo watu wamezisifu katika wimbo.
25 Wanadamu wote wameiona;
watu wanaikazia macho kwa mbali.
26 Tazama jinsi Mungu alivyo mkuu,
kupita ufahamu wetu!
Hesabu ya miaka yake haitafutiki.

27 “Yeye huvuta juu matone ya maji,
ayachujayo kama mvua kutoka vijito;
28 mawingu huangusha chini maji yake,
nayo mvua nyingi huwanyeshea wanadamu.
29 Ni nani ajuaye jinsi ayatandazavyo mawingu,
jinsi angurumavyo kutoka kwenye hema lake.
30 Tazama anavyotandaza radi yake kumzunguka,
naye huvifunika vilindi vya bahari.
31 Hivi ndivyo atawalavyo mataifa,
na kuwapa chakula kwa wingi.
32 Huujaza mkono wake kwa radi,
na kuiagiza kulenga shabaha yake.
33 Ngurumo zake hutangaza dhoruba inayokuja;
hata mifugo hujulisha kukaribia kwake*.

# 37

## *Elihu atukuza maajabu ya Mwenyezi Mungu*

* **36:33** au *hutangaza kuja kwake*

1 “Kwa hili moyo wangu unatetemeka,
nao unaruka kutoka mahali pake.
2 Sikiliza! Sikiliza ngurumo ya sauti yake,
sauti ya ngurumo inayotoka kinywani mwake.
3 Huuachilia umeme wake wa radi chini ya mbingu yote
na kuupeleka hata miisho ya dunia.
4 Baada ya hayo huja sauti ya ngurumo yake;
Mungu hunguruma kwa sauti yake ya fahari.
Wakati sauti yake inanguruma tena,
huuachilia umeme wake wa radi.
5 Sauti ya Mungu hunguruma kwa namna za ajabu;
yeye hutenda mambo makuu kupita ufahamu wetu.
6 Huiambia theluji, ‘Anguka juu ya dunia,’
nayo manyunyu ya mvua, ‘Uwe mvua ya nguvu.’
7 Ili wanadamu wote aliowaumba wapate kujua kazi zake,
yeye humzuilia kila mtu shughuli zake.
8 Wanyama hujificha;
hubakia kwenye mapango yao.
9 Dhoruba hutoka katika chumba chake,
baridi hutoka katika upepo uendao kasi.
10 Pumzi ya Mungu hutoa barafu,
eneo kubwa la maji huganda.
11 Huyasheheneza mawingu kwa maji,
naye husambaza umeme wake wa radi kupitia hayo.
12 Nayo mawingu huzungukazunguka pande zote kwa amri yake,

juu ya uso wa dunia yote,
kufanya lolote ayaamuruyo.
13 Huleta mawingu ili kuadhibu wanadamu,
au kuinyeshea dunia yake na kuonesha upendo wake.

14 “Ayubu, sikiliza hili;
nyamaza na uyafikiri maajabu ya Mungu.
15 Je, unajua jinsi Mungu anavyoyaongoza mawingu,
na kufanya umeme wake wa radi utoe mwanga?
16 Je, unajua mawingu yanavyokaa yakiwa yametulia,
hayo maajabu yake yeye aliye mkamilifu katika maarifa?
17 Wewe unayeshindwa na joto katika nguo zako
wakati nchi imenyamazishwa kimya bila upepo wa kusini,
18 je, unaweza kuungana naye katika kuzitandaza anga,
zilizo ngumu kama kioo cha shaba ya kuyeyushwa?

19 “Tuambieni yatupasayo kumwambia;
hatuwezi kutayarisha shauri letu kwa sababu ya ujinga wetu.
20 Je, aambiwe kwamba nataka kuongea?
Je, yuko mtu ambaye angeomba kumezwa?
21 Basi hakuna awezaye kulitazama jua,
jinsi linavyong’aa angani,
upepo ukishafagia mawingu.
22 Kutoka kaskazini yeye huja na fahari kuu;

Mungu huja katika utukufu wa kutisha.
23 Yeye Mwenyezi hatuwezi kumfikia,
naye ametukuzwa katika uweza;
katika hukumu zake na haki yake kuu,
hatadhulumu.
24 Kwa hiyo wanadamu humwogopa,
kwa kuwa yeye hamstahi yeyote
anayejidhania kuwa ana hekima.”

# Sehemu ya nne: Mwenyezi Mungu anazungumza

## 38

*(Ayubu 38–41)*

*Mwenyezi Mungu amjibu Ayubu*

1 Kisha Mwenyezi Mungu akamjibu Ayubu ku-
toka upepo wa kisulisuli. Akasema:
2 “Nani huyu atiaye mashauri yangu giza
kwa maneno yasiyo na maarifa?
3 Jikaze kama mwanaume;
nitakuuliza swali,
nawe unijibu.

4 “Ulikuwa wapi nilipoweka misingi ya dunia?
Niambie, kama unafahamu.
5 Ni nani aliyeweka alama vipimo vyake?
Hakika wewe unajua!
Ni nani aliyenyoosha kamba ya kupimia juu
yake?
6 Je, misingi yake iliwekwa juu ya nini,
au ni nani aliyeweka jiwe la pembeni,
7 wakati nyota za asubuhi zilipoimba pamoja,

na malaika wote walipokuwa wakishangilia
kwa furaha?

8 “Ni nani aliyeifungia bahari milango
ilipopasuka kutoka tumbo,
9 nilipoyafanya mawingu kuwa vazi lake,
na kuyafungia katika giza nene,
10 nilipoamuru mipaka yake,
na kuiweka milango yake na makomeo mahali pake,
11 niliposema, ‘Unaweza kufika hapa, wala si zaidi;
hapa ndipo mawimbi yako yenye kiburi yatakapokomea’?

12 “Umepata kuiamrisha asubuhi ipambazuke,
au kuyaonesha mapambazuko mahali pake,
13 yapate kushika miisho ya dunia,
na kuwakung’uta waovu waliomo?
14 Dunia hubadilika kama udongo wa mfinyanzi chini ya muhuri;
sura yake hukaa kama ile ya vazi.
15 Waovu huzuiliwa nuru yao,
nao mkono wao ulioinuliwa huvunjwa.

16 “Je, umepata kufika kwenye chemchemi za bahari?
Au kutembea mahali pa ndani pa vilindi?
17 Umewahi kuoneshwa malango ya mauti?
Umewahi kuiona milango ya uvuli wa mauti?
18 Je, wewe unafahamu ukubwa wa dunia?
Niambie kama unajua haya yote.

19 “Njia ya kufika kwenye makao ya nuru ni ipi?
Nako maskani mwa giza ni wapi?
20 Je, unaweza kuvirudisha kwenye makao yake?
Unajua njia za kufika maskani mwake?
21 Hakika unajua, kwa kuwa ulikuwa umeshazaliwa!
Kwani umeishi miaka mingi!

22 “Je, umeshawahi kuingia katika maghala ya theluji,
au kuona maghala ya mvua ya mawe,
23 ambazo nimeziweka akiba kwa ajili ya wakati wa taabu,
na kwa ajili ya wakati wa vita na mapigano?
24 Njia iendayo mahali miali ya radi inapotawanywa ni ipi,
au njia iendayo mahali upepo wa mashariki unaposambazwa juu ya dunia?
25 Ni nani aliyepasua mifereji kwa ajili ya maji mengi ya mvua yaendayo kasi
na njia ya miali ya radi,
26 ili kusababisha mvua kunyeshea mahali pasipokaliwa na mtu,
jangwa lisilo na yeyote ndani yake,
27 ili kuitosheleza nchi ya ukiwa na jangwa,
na majani yaanze kumea ndani yake?
28 Je, mvua ina baba?
Ni nani baba azaaye matone ya umande?
29 Barafu inatoka tumbo la nani?
Ni nani azaaye ukungu kutoka mbinguni,
30 wakati maji yanakuwa magumu kama jiwe,
wakati uso wa vilindi vya maji unaganda?

31 “Je, unaweza kuufunga mnyororo wa Kilimia?
Unaweza kulegeza kamba za Orioni?
32 Unaweza kuyaongoza makundi ya nyota kwa majira yake,
au kuongoza Dubu na watoto wake?
33 Je, unajua sheria zinazotawala mbingu?
Unaweza kuweka utawala wa Mungu duniani?

34 “Unaweza kuipaza sauti yako hadi mawinguni,
na kujifunika mwenyewe na gharika ya maji?
35 Je, wewe hutuma miali ya radi kwenye njia zake?
Je, hutoa taarifa kwako kukuambia, ‘Sisi tuko hapa’?
36 Ni nani aliyeujalia moyo hekima
au kuzipa akili ufahamu?
37 Nani mwenye hekima ya kuyahesabu mawingu?
Ni nani awezaye kuinamisha magudulia ya mbinguni
38 mavumbi yanapokuwa magumu,
na mabonge ya udongo kushikamana pamoja?

39 “Je, utamwindia simba jike mawindo,
na kuwashibisha simba wenye njaa
40 wakati wao wamejikunyata mapangoni mwao,
au wakivizia kichakani?
41 Ni nani ampaye kunguru chakula
wakati makinda yake yanamlilia Mungu,

yakizungukazunguka kwa ajili ya kukosa chakula?

# 39

*Mwenyezi Mungu anaendelea kumjibu Ayubu*

1 “Je, unajua wakati mbuzi wa mlimani wanapozaa?
Je, unatambua wakati kulungu jike anapozaa mtoto wake?
2 Je, unaweza kuhesabu miezi hadi wanapozaa?
Je, unajua majira yao ya kuzaa?
3 Wao hujiinamisha na kuzaa watoto wao;
uchungu wa kuzaa unakoma.
4 Watoto wao hustawi na kuongezeka nguvu nyikani;
huenda zao wala hawarudi tena.

5 “Ni nani aliyemwachia punda-mwitu awe huru?
Ni nani aliyezifungua kamba zake?
6 Nimempa nchi isiyokaliwa na watu kuwa masikani yake,
nchi ya chumvi kuwa makao yake.
7 Huzicheka ghasia za mji,
wala hasikii kelele za mwendesha gari.
8 Huzunguka vilimani kwa ajili ya malisho
na kutafuta kila kitu kibichi.

9 “Je, nyati atakubali kukutumikia?
Atakaa karibu na hori lako usiku?
10 Je, unaweza kumfungia kwenye matuta kwa kamba?
Je, atalima mabonde nyuma yako?

11 Je, utamtumainia kwa ajili ya nguvu zake nyingi?
Utamwachia yeye kazi zako nzito?
12 Utaweza kumwamini akuletee nafaka yako nyumbani
kutoka shambani na kuikusanya kwenye sakafu yako ya kupuria?

13 “Mbuni hupigapiga mabawa yake kwa furaha,
lakini hayawezi kulinganishwa
na mabawa na manyoya ya korongo.
14 Huyataga mayai yake juu ya ardhi,
na kuyaacha yapate joto mchangani,
15 bila kujali kuwa mguu unaweza kuyaponda,
kwamba baadhi ya wanyama wa porini wanaweza kuyakanyaga.
16 Yeye huyafanyia makinda yake ukatili kama vile si yake;
hajali kwamba taabu yake inaweza ikawa bure,
17 kwa kuwa Mungu hakumjalia hekima,
wala hakumpa fungu la akili njema.
18 Lakini akunjuapo mabawa yake kukimbia,
humcheka farasi pamoja na yeye aliyempanda.

19 “Je, wewe humpa farasi nguvu
au kuivika shingo yake manyoya marefu?
20 Je, wewe humfanya farasi aruke kama nzige,
akistaajabisha kwa tishio la mlio wake wa majivuno?
21 Huparapara bila woga, akizifurahia nguvu zake,

husonga mbele kukabiliana na silaha.
22 Huicheka hofu, haogopi chochote,
wala haukimbii upanga.
23 Podo hutoa sauti kando yake,
pamoja na mkuki unaong'aa na fumo.
24 Bila woga na kwa ghadhabu huimeza nchi,
wala tarumbeta iliapo yeye hawezi kusimama.
25 Asikiapo sauti ya baragumu yeye hulia, 'Aha!'
Hunusa harufu ya vita toka mbali,
husikia sauti ya mtoa amri na kelele za vita.

26 "Je, mwewe huruka kwa hekima yako
na kuyakunjua mabawa yake kuelekea kusini?
27 Je, tai hupaa juu kwa amri yako
na kujenga kiota chake mahali pa juu?
28 Huishi juu ya miamba mirefu na kukaa huko usiku;
majabali yenye ncha kali ndiyo ngome yake.
29 Kutoka huko hutafuta chakula chake;
macho yake hukiona kutoka mbali.
30 Makinda yake hujilisha damu,
na pale palipo na machinjo, ndipo yeye alipo."

# 40

*Mwenyezi Mungu anamuuliza Ayubu maswali*

1 Mwenyezi Mungu akamwambia Ayubu:
2 "Je, mwenye kushindana na Mwenyezi aweza kumsahihisha?
Mwenye kumlaumu Mungu na ajibu."
3 Ndipo Ayubu akamjibu Mwenyezi Mungu:

4 “Mimi sistahili kabisa: ninawezaje kukujibu wewe?
Nauweka mkono wangu juu ya kinywa changu.
5 Nimesema mara moja, lakini sina jibu;
naam, nimesema mara mbili,
lakini sitasema tena.”
6 Ndipo Mwenyezi Mungu akasema na Ayubu
kutoka upepo wa kisulisuli:
7 “Jikaze kama mwanaume;
nitakuuliza maswali, nawe yakupasa unijibu.

8 “Je, utabatilisha hukumu yangu?
Utanilaumu mimi ili kujihesabia haki mwenyewe?
9 Je, una mkono kama wa Mungu,
nawe unaweza kutoa sauti ya ngurumo kama yake?
10 Basi jivike mwenyewe utukufu na fahari,
nawe uvae heshima na enzi.
11 Fungulia ukali wa ghadhabu yako,
mtafute kila mwenye kiburi umshushe,
12 mwangalie kila mtu mwenye kiburi na umnyenyekeze,
waponde waovu mahali wasimamapo.
13 Wazike wote mavumbini pamoja;
wafunge nyuso zao kaburini.
14 Ndipo mimi mwenyewe nitakukubalia
kuwa mkono wako mwenyewe wa kuume unaweza kukuokoa.

15 “Mwangalie mnyama aitwaye Behemothi*,
niliyemuumba kama nilivyokuumba wewe,
anayekula majani kama ng'ombe.
16 Tazama basi nguvu alizo nazo kwenye viuno vyake,
uwezo alio nao kwenye misuli ya tumbo lake!
17 Mkia wake hutikisika kama mwerezi;
mishipa ya mapaja yake imesukwa pamoja.
18 Mifupa yake ni bomba za shaba,
maungo yake ni kama fito za chuma.
19 Yeye ni wa kwanza miongoni mwa kazi za Mungu,
lakini Muumba wake anaweza kumsogelea kwa upanga wake.
20 Vilima humletea yeye mazao yake,
nao wanyama pori wote hucheza karibu naye.
21 Hulala chini ya mimea ya yungiyungi,
katika maficho ya matete kwenye matope.
22 Hiyo mimea ya yungiyungi humficha kwenye vivuli vyake;
miti mirefu karibu na kijito humzunguka.
23 Mto unapofurika,
yeye hapati mshtuko wa hofu;
yeye yu salama, hata kama Yordani ingefurika
hadi kwenye kinywa chake.
24 Je, mtu yeyote anaweza kumkamata yeye akiwa macho,
au kumnasa kwa mtego na kutoboa pua yake?

* **40:15** Behemothi alikuwa mnyama wa nyakati za zamani ambaye hajulikani hasa ni gani.

# 41

## *Mwenyezi Mungu anaendelea kumuuliza Ayubu maswali*

1 “Je, unaweza kumvua Lewiathani* kwa ndoana ya samaki,
au kufunga ulimi wake kwa kamba?
2 Unaweza kupitisha kamba puani mwake,
au kutoboa taya lake kwa kulabu?
3 Je, ataendelea kukuomba umhurumie?
Atasema nawe maneno ya upole?
4 Je, atafanya agano nawe ili umtwae
awe mtumishi wako maisha yake yote?
5 Je, utamfuga na kumfanya rafiki kama ndege,
au kumfunga kamba kwa ajili ya wasichana wako?
6 Je, wafanyabiashara watabadilishana bidhaa kwa ajili yake?
Watamgawanya miongoni mwa wafanyao biashara?
7 Je, unaweza kuijaza ngozi yake kwa vyuma vyenye ncha kali,
au kichwa chake kwa mkuki wa kuvulia samaki?
8 Ukiweka mkono wako juu yake,
utavikumbuka hivyo vita na kamwe hutarudia tena!
9 Tumaini lolote la kumtiisha ni kujidanganya;
kule kumwona tu kunamwangusha mtu chini.

---

* **41:1** Lewiathani ni mnyama mkubwa wa baharini mwenye magamba anayefanana na joka kubwa, mwenye umbo la kutisha, asiyeweza kuvuliwa.

10 Hakuna yeyote aliye mkali athubutuye kumchokoza.
Ni nani basi awezaye kusimama dhidi yangu?
11 Ni nani mwenye madai dhidi yangu ili nipate kumlipa?
Kila kitu kilicho chini ya mbingu ni mali yangu.

12 “Sitashindwa kunena kuhusu maungo yake,
nguvu zake na umbo lake zuri.
13 Ni nani awezaye kumvua gamba lake la nje?
Ni nani awezaye kumsogelea na lijamu?
14 Nani athubutuye kuufungua mlango wa kinywa chake,
kilichozungukwa na meno yake ya kutisha pande zote?
15 Mgongo wake una safu za ngao
zilizoshikamanishwa imara pamoja;
16 kila moja iko karibu sana na mwenzake,
wala hakuna hewa iwezayo kupita kati yake.
17 Zimeunganishwa imara kila moja na nyingine;
zimeng’ang’aniana pamoja wala haziwezi kutenganishwa.
18 Akipiga chafya mwanga humetameta;
macho yake ni kama miali ya mapambazuko.
19 Mienge iwakayo humiminika kutoka kinywani mwake;
cheche za moto huruka nje.
20 Moshi hufuka kutoka puani mwake,
kama kutoka chungu kinachotokota kwa moto wa matete.
21 Pumzi yake huwasha makaa ya mawe,

nayo miali ya moto huruka kutoka kinywani mwake.
22 Nguvu hukaa katika shingo yake;
utisho hutangulia mbele yake.
23 Mikunjo ya nyama yake imeshikamana imara pamoja;
iko imara na haiwezi kuondolewa.
24 Kifua chake ni kigumu kama mwamba,
kigumu kama jiwe la chini la kusagia.
25 Ainukapo, mashujaa wanaogopa;
wanarudi nyuma mbele ya kishindo chake.
26 Upanga unaomfikia haumdhuru,
wala mkuki au mshale wala fumo.
27 Chuma hukiona kama unyasi,
na shaba kama mti uliooza.
28 Mishale haimfanyi yeye akimbie;
mawe ya kombeo kwake ni kama makapi.
29 Rungu kwake huwa kama kipande cha jani kavu;
hucheka sauti za kugongana kwa mkuki.
30 Sehemu zake za chini kwenye tumbo
zina menomeno na mapengo kama vigae vya chungu,
zikiacha mburuzo kwenye matope
kama chombo chenye meno cha kupuria.
31 Huvisukasuka vilindi kama sufuria kubwa ichemkayo,
na kukoroga bahari kama chungu cha marhamu.
32 Anapopita nyuma yake huacha mkondo unaometameta;
mtu angedhani vilindi vilikuwa na mvi.
33 Hakuna chochote duniani kinacholingana naye:

yeye ni kiumbe kisicho na woga.
34 Yeye huwatazama chini wale wote wenye kujivuna;
yeye ni mfalme juu ya wote wenye kiburi."

# Sehemu ya tano

## 42

*(Ayubu 42)*

### *Ayubu anamjibu Mwenyezi Mungu*

1 Ndipo Ayubu akamjibu Mwenyezi Mungu:
2 "Ninajua ya kuwa unaweza kufanya mambo yote,
wala hakuna mpango wako unaoweza kuzuilika.
3 Uliuliza, 'Ni nani huyu
afichaye mashauri yangu
bila maarifa?'
Hakika nilisema mambo nisiyoyaelewa,
mambo ya ajabu mno
kwangu mimi kuyajua.

4 "Ulisema, 'Sikiliza sasa, nami nitanena;
nitakuuliza swali, nawe yakupasa kunijibu.'
5 Masikio yangu yalikuwa yamesikia habari zako,
lakini sasa macho yangu yamekuona.
6 Kwa hiyo najidharau mwenyewe,
na kutubu katika mavumbi na majivu."

### *Mwisho: Rafiki zake Ayubu wanafedheheshwa*

7 Baada ya Mwenyezi Mungu kusema mambo
haya yote na Ayubu, akamwambia Elifazi Mte-
mani, "Nina hasira nawe na rafiki zako wawili,

kwa sababu hamkusema yaliyo sawa kunihusu,
kama alivyosema mtumishi wangu Ayubu.
8 Basi sasa chukueni mafahali saba na kon-
doo dume saba mkamwendee mtumishi wangu
Ayubu nanyi mkatoe sadaka za kuteketezwa
kwa ajili yenu wenyewe. Mtumishi wangu
Ayubu atawaombea, nami nitayakubali maombi
yake ili nisiwatendee sawasawa na upumbavu
wenu. Ninyi hamkusema yaliyo sawa kwa
habari yangu, kama alivyosema mtumishi wangu
Ayubu."
9 Kwa hiyo Elifazi Mtemani, Bildadi Mshuhi, na
Sofari Mnaamathi wakafanya kama Mwenyezi
Mungu alivyowaambia; naye Mwenyezi Mungu
akayakubali maombi ya Ayubu.
10 Baada ya Ayubu kuwaombea rafiki zake,
Mwenyezi Mungu akamwondoa kwenye uteka,
akamfanikisha tena naye akampa mara mbili ya
vile alivyokuwa navyo hapo mwanzoni.
11 Ndipo ndugu zake na dada zake wote, na kila
mtu aliyemfahamu mwanzoni wakaja, wakala
pamoja naye katika nyumba yake. Wakamfariji
na kumtuliza moyo juu ya taabu yote Mwenyezi
Mungu aliyoileta juu yake, nao kila mmoja
akampa kipande cha fedha na pete ya dhahabu.
12 Mwenyezi Mungu akaibariki sehemu ya
mwisho ya maisha ya Ayubu kuliko ile ya
kwanza. Alikuwa na kondoo elfu kumi na nne,
ngamia elfu sita, jozi za mafahali elfu moja, na
punda jike elfu moja.
13 Tena alikuwa na wana saba na binti watatu.
14 Binti wa kwanza aliitwa Yemima, wa pili
Kesia, na wa tatu Keren-Hapuki.

15 Katika nchi ile yote hakukuwa wanawake
wazuri kama binti za Ayubu; naye baba yao
akawapa urithi pamoja na ndugu zao.
16 Baada ya hili Ayubu akaishi miaka mia moja
na arobaini; akawaona wanawe, na wana wa
wanawe hata kizazi cha nne.
17 Hivyo Ayubu akafa, akiwa mzee aliyeshiba
siku.

# Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu

## The Holy Bible in Swahili: Open Neno: Maandiko Matakatifu 2024

copyright © 2018, 2024 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili (Swahili)

Contributor: Biblica, Inc.

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

**Creative Commons License**

Kazi hii imewezeshwa kupitia idhini ya kundi la the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). Ili kuona nakala ya idhini hii, angalia kwenye anwani tovuti ya http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 au uandike barua kwa Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® ni alama ya biashara iliyosajilishwa na shirika la Biblica, Inc; unahitaji ruhusa ya kimaandiko kutoka kwa Biblica, Inc. ili kutumia alama ya biashara ya Biblica®. Kulingana na makubaliano ya leseni ya CC BY-SA, unaweza kutoa nakala na kusambaza kazi hii bila kuibadilisha kamwe, mradi tu udumishe alama ya biashara ya Biblica®. Ukibadilisha au kufasiri kazi hii, na hivyo ukanyambua kazi tofauti, sharti uondoe alama ya biashara ya Biblica®. Katika kazi uliyonyambua, sharti uarifu mabadiliko yako, na kutambua kazi yako hivi: "Kazi ya asili ya Biblica, Inc. inapatikana bila bei katika tovuti zawww.biblica.com na open.bible."

Ilani ya hakimiliki sharti iwe katika ukurasa wa kichwa au wa hakilimiliki kama ifuatavyo:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

Sharti pia uwasilishe kazi uliyonyambua kupitia kwa liseni hiyo hiyo ya CC BY-SA.

Ikiwa ungependa kujulisha Biblica, Inc. kuhusu tafsiri yako ya kazi hii, tafadhali wasiliana nasi katika tovuti https://open.bible/contact-us.

This work is made available under the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). To view a copy of this license, visit http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 or send a letter to Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® is a trademark registered by Biblica, Inc., and use of the Biblica® trademark requires the written permission of Biblica, Inc. Under the terms of the CC BY-SA license, you may copy and redistribute this unmodified work as long as you keep the Biblica® trademark intact. If you modify a copy or translate this work, thereby creating a derivative work, you must remove the Biblica® trademark. On the derivative work, you must indicate what changes you have made and attribute the work as follows: "The original work by Biblica, Inc. is available for free atwww.biblica.com and open.bible."

Notice of copyright must appear on the title or copyright page of the work as follows:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

You must also make your derivative work available under the same license (CC BY-SA).

If you would like to notify Biblica, Inc. regarding your translation of this work, please contact us at https://open.bible/contact-us.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.

You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.

If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.

Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2025-05-21

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 20 May 2025 from source files dated 21 May 2025

72687ba8-7233-577d-bf23-786df16f869d